# ATHARI ZA UDHANAISHI KATIKA *KICHWAMAJI* NA *NGUVU YA SALA*

NA

NKONGE GAKII LILIAN

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A.) KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

MEI, 2006

JOMO KENYATTA MEMORIAL
LIBRARY

University of NAIROBI Library
0496801 2

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine.

LILIAN G. NKONGE

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

DKT. MWENDA MBATIAH

DKT. KINEENE WA MUTISO

## TABARUKU

Tasnifu hii namtabarukia marehemu babangu, JOHN NKONGE kwa kunitia ari ya masomo ningali mtoto mdogo,

na

Mamangu mpenzi, HARRIET NYOROKA, asiyechoka kamwe kuniombea na kunihimiza.

## SHUKRANI

Nawajibika kumshukuru Maulana kwa kuniwezesha kuikamilisha kazi hii licha ya changamoto za hapa na pale.

Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu. Dkt. Mwenda Mbatiah na Dkt. Kineene wa Mutiso ambao hawakuchoka kuipitia kazi hii. Ushauri wao ulinifaa sana hasa wakati mawazo yangu yalikuwa yamevurugika. Vilevile nawashukuru wahadhiri wengine wa Kiswahili ambao ni Bi Mwaliwa, Bi. Njuguna, Dkt. Olali, Dkt. Kithaka, Dkt. Habwe na Prof. Abdulaziz. Prof. Omondi pia hawezi kusahaulika.

Nawanyooshea mkono wa shukrani wazazi wangu, John na Harriet, kwa kujinyima mengi kusudi waniwekee msingi imara wa masomo na maisha pia. Bila msingi huo ingeniwia vigumu kusoma hadi kiwango hiki. Daima nitabaki na deni la wema wenu.

Aidha ninawashukuru ndugu zangu, Ayub Mwongera, Julius Mutwiri, Zippy Micheni na Doreen Makena, ambao walisimama pamoja nami kwa hali na mali wakati wa masomo yangu. Siwezi kuwasahau wapwa wangu; Prudence Kinya, Kendi, Gatwiri, Kawira, Mwende, Kagendo, Murithi, Kirimi na Duncan Mugambi. Someni kwa bidii.

Sina budi kuwashukuru wenzangu tuliodurusu nao, pamoja na kwamba walikuwa marafiki wa karibu. Hawa ni Fridah Kaviti, Veronica Maina, Eddah Wanja na Julius Mungai. Wengine ni, Assumpta, Mary, Rukia, Njiru, Theuri, Meddy, Wepo, Mungai, Nyabunga, na Kyalo Nguku. Mlionihimiza wakati wa dhiki, asanteni sana.

Nitakosea nisipowashukuru Bi na Bw. Joel, Stella Nkaabu, Bi Mwende Andrew, Irungu, Peter, Grace Wanja, Bi na Bw. Thilange na Bi na Bw. Kimathi. Hisani yao kwangu haiwezi kusahaulika kamwe.

Ni muhali kumsahau Racheal ambaye aliichapa kazi hii kwa ustadi. Ama kweli, ni wengi sana walionifaa katika kuikamilisha kazi hii. Kuwataja wote kutagharimu kurasa nyingi. Hata hivyo kwa wote niliowataja na wale ambao sikuwataja, ninasema mpokee shukrani zangu za dhati.

Kwenu nyote, Mungu awabariki na awaonee wema katika dunia hii iliyojaa usumbufu.

# IKISARI

Tasnifu hii imechunguza athari za udhanaishi katika riwaya mbili ambazo ni *Kichwamaji* na *Nguvu ya Sala*. Kazi yenyewe imegawika katika sura nne.

Katika sura ya kwanza tumetanguliza kwa ufupi dhana ya udhanaishi. Vilevile, tumebainisha tatizo linalotafitiwa, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, pamoja na njia za utafiti. Aidha tumeangazia udurusu wa kazi mbalimbali pamoja na msingi wa kinadharia. Tumetumia nadharia ya kisosholojia inayosisitiza umuhimu wa mazingira yaliyoibusha kazi ya msanii.

Katika sura ya pili, tumeonyesha athari za udhanaishi zinazobainika katika riwaya ya *Kichwamaji.* Vilevile mazingira mbalimbali ambayo yamemwathiri Kezilahabi na kumfanya achukue mtazamo wa kidhanaishi yamejadiliwa.

Sura ya tatu imeangazia udhanaishi katika *Nguvu ya Sala*. Tumebainisha athari za udhanaishi kupitia maudhui mbalimbali. Aidha tumeonyesha vile ambavyo mwandishi ameathiriwa na mazingira alimoandikia.

Sura ya nne ni hitimisho. Tumehitimisha kwa kutoa maoni kuhusiana na kazi hii kwa ujumla. Vilevile, tumetoa mapendekezo ya utafiti zaidi.

## FARAHASA

UNGAMO ........................................................................................................i

TABARUKU ........................................................................................................ii

SHUKRANI ........................................................................................................iii

IKISARI ........................................................................................................v

FARAHASA ........................................................................................................vi

SURA YA KWANZA ........................................................................................................1

1.0 USULI ........................................................................................................1

1.1 UTANGULIZI ........................................................................................................1

1.2 TATIZO LINALOTAFITIWA ........................................................................................................4

1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI ........................................................................................................5

1.4 NADHARIA TETE ........................................................................................................5

1.5 MIPAKA NA UPEO ........................................................................................................5

1.6 SABABU ZA KULICHAGUA TATIZO HILI ........................................................................................................5

1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII ........................................................................................................6

1.8 MSINGI WA KINADHARIA ........................................................................................................7

1.9 NJIA ZA UTAFITI ........................................................................................................9

TANBIHI ........................................................................................................10

SURA YA PILI ........................................................................................................11

2.0 ATHARI ZA UDHANAISHI KATIKA ***KICHWAMAJI*** ........................................................................................................11

2.1 UTANGULIZI ........................................................................................................11

2.2 MAUDHUI ....................................................................................................11
2.2.1 Elimu na Utamaduni ....................................................................................11
2.2.2 Mapenzi na Ndoa ........................................................................................16
2.2.3 Maisha na Kifo............................................................................................20
2.2.4 Dini ............................................................................................................25
2.2.5 Maisha ya Vijijini na Mijini...........................................................................28
2.3 KUATHIRIWA KWA MWANDISHI NA MAZINGIRA MBALIMBALI..................32
2.4 HITIMISHO..................................................................................................38
SURA YA TATU ..............................................................................................39
3.0 UDHANAISHI KATIKA ***NGUVU YA SALA***..........................................................*39*
3.1 UTANGULIZI ...............................................................................................39
3.2 MAUDHUI ....................................................................................................39
3.2.1 Malezi ........................................................................................................39
3.2.2 Uozo wa Jamii..............................................................................................45
3.2.3 Dhana ya Maisha..........................................................................................48
3.2.4 Dini ............................................................................................................56
3.2.5 Kifo ............................................................................................................62
3.3 ATHARI YA MAZINGIRA KWA MWANDISHI ...................................................63
3.4 HITIMISHO...................................................................................................66
SURA YA NNE.................................................................................................68
4.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....................................................................68
4.1 HITIMISHO...................................................................................................68
4.2 MAPENDEKEZO.............................................................................................69
MAREJELEO ...................................................................................................71

# SURA YA KWANZA

# USULI

## 1.0 UTANGULIZI

Udhanaishi ni falsafa ambayo inajishughulisha na maisha ya binadamu. Wanaudhanaishi humwona binadamu kama kiumbe pweke aliyetupwa katika ulimwengu unaomtesa. Katika kujishughulisha na maisha ya binadamu, wanaudhanaishi hutilia maanani tajriba za mtu binafsi katika safari yake ya maisha. Udhanaishi ulianzia katika mataifa ya Kimagharibi, muda mfupi tu baada ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia. Ulikuwa na athari kubwa nchini Ufaransa na Ujerumani kabla ya kuenea sehemu nyinginezo. Ingawa wanahistoria hutofautiana kuhusu mwasisi wa falsafa hii, inaaminika kuwa iliasisiwa na watu kama St. Augustine, Duns Scotus, na Pascal Blaise.

Hata hivyo, wengi wanakubaliana kuwa Soren Kierkegaard ndiye mwasisi wa udhanaishi wa kisasa[1]. Vitabu vyake kama vile; the *Concept of Dread, Fear and Trembling* na *Sickness unto Death,* viliwekea falsafa hii msingi thabiti. Kierkegaard ndiye aliyeunda dhana na msamiati uliowaathiri wafuasi wa udhanaishi. Katika karne ya ishirini udhanaishi ulipata wafuasi kama vile Martin Heidegger, Friedrich Nietzsche, na Karl Jaspers. Baadaye, Jean – Paul Sartre, Franz Kafka na Albert Camus walijitokeza na kazi ambazo ziliusambaza udhanaishi na zikaathiri wasanii wengi.

Kuna matapo mawili ya udhanaishi. Tapo moja ni lile la Kikristo. Hili lina misingi yake katika mawazo ya mwanafalsafa Gabriel Marcel[2]. Greene (1990:61) anaeleza kuwa Gabriel Marcel, ndiye kiongozi wa udhanaishi wa Kikristo. Udhanaishi wa Kilimwengu au wa Ukanaji Mungu ndilo tapo la pili la udhanaishi. Jean –Paul Sartre, mwanafalsafa wa Kifaransa, ndiye anayesifika kama kiongozi wa udhanaishi wa Kilimwengu[3]. Greene (1960:61) anaendelea kueleza kwamba Satre aliposhuka kutoka kwa ndege aliwashangaza waandishi wa habari aliposema kuwa 'Mungu amekufa.' Jean-Paul Sartre, kiongozi wa kundi la udhanaishi wa kilimwengu alinukuliwa na Pasquier (1950) akisema:

> Udhanaishi ambao awali ulihusishwa na Kierkegaard, ulienda sambamba na imani za kidini. Udhanaishi wa Kifaransa leo huelekea kuhusishwa na kutosadiki kuwa Mungu yuko. ..

Wengine wanaohusishwa na udhanaishi wa Kilimwengu ni kama vile; Samwel Beckett, Georges Bataille na Simone de Beauvoir. Tapo hili hudadisi kuwepo kwa Mungu.

Vilevile Friedrich Nietzsche, mwanaudhanaishi aliyeandika *Thus Spake Zarathustra* na *The Will to Power* alidai kuwa "kanisa ni kaburi la Mungu". Nietzshche pia alijulikana kwa tamko lake maarufu katika *Joyful Wisdom* kuwa 'Mungu amekufa'.[4] Ingawa udhanaishi wa Kikristo ndio mkongwe kuliko ule wa Kilimwengu, [5] udhanaishi wa Kilimwengu ndio ambao umeendelea sana. Maendeleo hayo yanahusishwa na Jean-Paul Sartre. Mawazo haya yanaafikiana na ya Kaufmann (1956:40) anaposema kuwa udhanaishi umesambaa sana kimataifa kupitia kazi za Jean-Paul Sartre.

Udhanaishi una vipengele muhimu ambavyo vinadhihirika katika kazi mbaslimbali za waandishi ambao wanaegemea falsafa ya udhanaishi. Wadhanaishi wengi hutilia mkazo mateso yanayomkumba binadamu. Wao humwona binadamu kama kiumbe pweke aliyetupwa katika ulimwengu katili ambamo hujaribu kutimiza malengo yake. Suala la binadamu na maisha yake magumu katika ulimwengu unaomtesa linaendelezwa na Greene (1960:9) anapoeleza kuwa kuteseka na kuhisi maumivu kwa binadamu ni hali ambayo haiwezi kuepukika ulimwenguni.

Swala la Mungu ni kipengele muhimu cha udhanaishi. Kuna wanaodadisi kuwepo kwa Mungu. Pascal Blaise ambaye amenukuliwa na Foulquie (1948) aliandika na kuuliza, 'Mungu anaishi au la? Tunawezaje kuamua?' Kulingana na *The New Columbia Encyclopaedia* (1975) Jean-Paul Sartre, kiongozi wa Udhanaishi wa Kilimwengu alidai kuwa hakuna Mungu. Aliamini kuwa binadamu aliweza kujiamulia bila kumtegemea Mungu. Mawazo haya yanatiliwa mkazo na Wilson na Goldfarb (1991:402) wanaposema kuwa Mungu hayuko na hivyo binadamu yu pekee

katika ulimwengu katili. Kiudhanaishi, wazo la Mungu humjia binadamu baada ya kushindwa kukabiliana na maisha yake.

Aidha kuna maelezo kuwa mwanadamu hana uwezo juu ya maisha yake. Matukio maishani, kama vile ajali hutukia tu bila kutarajiwa. Kwake binadamu, maisha ni kama mtego ambao umemnasa lakini kwa kuwa yeye ni kiumbe dhaifu, hana namna ya kujinasua kutoka kwa mtego huo. Martin Heidegger alieleza kuwa binadamu analazimika kutegemea ajali ambayo ndiyo chanzo cha matukio maishani mwake, wala hawezi kuikwepa kwa vyovyote vile. Haya yanaafikiana na mawazo ya Warnock Mary aliyesisitiza kuwa juhudi za binadamu huwa bure kwani mwishoni, mtu hana budi kukikosa kile ambacho amekidhamiria.

Teneti nyingine ya udhanaishi ni kuwa kifo ni sehemu ya maisha ya binadamu. Binadamu hukabiliwa na kifo na huwa hana njia ya kujiepusha nacho. Kifo na maisha haviwezi kutenganishwa kwani kama anavyodai Samwel Beckett[7], maisha ni kuendelea kufa hadi kiwango kitakikanacho, ambacho ni kifo cha hakika. Hivyo basi, maisha yanaonekana kama kitendawili ambacho mwanadamu anapaswa kukitegua na akifaulu atakuwa amejua pia maana ya kifo. Mawazo haya yanapigiwa mwangwi na Lepp (1968: 139) anaposema:

> Badala ya kufikiria kifo kama mwisho wa maisha, ni heri tukitazame kama tukio la mwisho katika kutimiza maisha ya muda. Iwapo tutafaulu kuyapa maisha yetu maana, vivyo hivyo, kifo kitakuwa na maana. (Tafsiri yetu)

Suala la uhuru na umuhimu wa mtu binafsi linasisitizwa na wadhanaishi. Wanashikilia kuwa binadamu yu huru. Hata hivyo uhuru wenyewe si wa kufurahisha bali ni wa kuogofya. Hakuna cha kumsaidia mtu kuutumia uhuru wake au kufanya uamuzi ambao hana budi kuufanya. Uchaguzi unaweza kusababisha madhara yasiyoepukika. Aidha, Wamitila (2003:248) anasema kuwa sifa nyingine za udhanaishi ni ukengeushi na kihoro. Anaelezea kuwa maendeleo ya kisayansi na ya kitasnia ndiyo humkengeusha binadamu kutoka kwa Mungu, jamii na nafsi yake. Binadamu aliyekengeushwa huishia katika hali ya kihoro.

Aidha kuna kuzorota kwa maadili katika jamii. Mambo huwa yamevurugika na maovu kama vile ubakaji, ulevi, wizi, ukahaba, ufisadi na kadhalika huendelezwa na baadhi ya wanajamii. Vilevile ubatili wa maisha unatiliwa mkazo na wadhanaishi. Ionesco Eugene ambaye amenukuliwa na Wanjala (1978:7) anaonyesha ubatili wa maisha kwa kusema:

> Ninahisi kuwa maisha ni ndoto mbaya yenye uchungu usiostahimilika. Hebu tupa macho; vita, ajali, chuki, dhuluma majanga, kifo kinachotungojea kila upande... tunaumbwa tuishi lakini tunakufa. Maisha ni maafa. (Tafsiri yetu).

Ni kwa sababu hizi wanaudhanaishi hudadisi kuwepo kwa binadamu ulimwenguni. Kwao maisha katika ulimwengu uliojaa dhiki ni usumbufu usiokuwa na maana yoyote. Usumbufu huu humfanya binadamu akose furaha. Wanaudhanaishi hawaonyeshi uwezekano wa hali ya maisha ya binadamu kuwa bora hata katika siku za usoni. Hivyo maisha katika ulimwengu duni yanatamausha. Kama asemavyo Greene (1960:1) kinachotambulika ulimwenguni ni hali ya kukata tamaa, hofu na upweke wa kuweko kwa binadamu. Udhanaishi ni falsafa inayokatisha tamaa.

## 1.1 TATIZO LINALOTAFITIWA.

Tatizo letu hasa lilikuwa ni kuchunguza iwapo riwaya mbili ambazo ni *Kichwamaji* na *Nguvu ya Sala* zinaweza kuainishwa kama kazi za kidhanaishi. Udhanaishi uliozuka katika mataifa ya Ulaya ulisababisha uandishi wa fasihi iliyojulikana kama fasihi ya uduni. Waandishi wa fasihi ya Kiswahili wameandika kazi ambazo zinafuata mkondo huu wa uandishi. Athari na viwango vya udhanaishi katika kazi hizi ni suala ambalo lilihitaji kutafitiwa ili kujadili uwezekano wa msanii kuathiriwa na mazingira yake.

Tulichukulia kwamba mazingira ya kijamii yamewaathiri waandishi hawa, hasa kuhusiana na mwelekeo wao wa kiudhanaishi. Kwa sababu hii, udhanaishi katika kazi zinazohusika

ulichunguzwa kwa kuambatanishwa na mazingira ya kijamii wanamotoka waandishi wa kazi zilizohakikiwa.

## 1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

Madhumuni yetu katika utafiti huu yalikwa:

i) Kuchunguza udhanaishi katika riwaya ya *Nguvu ya Sala* na *Kichwamaji.*

ii) Kuchunguza namna mazingira ya kila mwandishi yalivyoathiri mtazamo wake wa kidhanaishi.

## 1.3 NADHARIA TETE

Utafiti huu ulikuwa na nadharia tete zifuatazo:

i) Kazi zote mbili zimesawiri athari za udhanaishi kupitia maudhui mbalimbali.

ii) Mazingira mbalimbali yameathiri mitazamo ya ki-udhanaishi ya waandishi wa kazi hizi.

## 1.4 MIPAKA NA UPEO

Utafiti huu umejikita katika riwaya mbili ambazo ni *Kichwamaji* na *Nguvu ya Sala.* Tumezihakiki kazi hizi ili kubainisha athari na viwango vya udhanaishi. Kazi yetu imeegemea zaidi upande wa maudhui. Hata hivyo,imegusia vipengele vya fani kama vile mandhari na lugha pale ambapo tumehisi vimechangia katika kubainisha udhanaishi. Pamoja na kwamba waandishi wa riwaya hizi ni wa kutajika katika tanzu zote za fasihi andishi, tumejikita zaidi katika riwaya tulizozitaja. Hata hivyo, tumezirejelea na kuzinukuu kazi nyingine zao pale ambapo zimetusaidia kutilia mkazo maswala ambayo tumeyashughulikia.

## 1.5 SABABU ZA KULICHAGUA TATIZO HILI

Tumechagua kulishughulikia tatizo hili kwa sababu ingawa falsafa ya udhanaishi ilianzia huko mataifa ya Magharibi, waandishi wa fasihi ya Kiswahili wameathiriwa nayo na wamejihusisha

na uandishi wa kazi zinazoegemea falsafa hiyo. Tumechagua kuhakiki riwaya ya *Kichwamaji* na *Nguvu ya Sala* kwa sababu waandishi wa kazi hizi ni mashuhuri katika uandishi wa fasihi ya Kiswahili. Vilevile, wametoka katika jamii tofauti. Hili litatusaidia katika kuchunguza namna mazingira yanavyoathiri kazi ya kila mwandishi. Ingawa kazi za Kezilahabi zimeshughulikiwa na mapana na marefu tunaamini kuwa hakuna uhakiki unaoweza kusemekana kuwa umekamilika. Wahakiki mbalimbali hutofautiana katika mitazamo yao. Vilevile, uhakiki hutegemea mabadiliko ya kijamii, kulingana na wakati kwa kuwa kazi hii ni linganishi ilitarajiwa kuwa itachangia katika kuonyesha ubia na upekee wa fasihi.

## 1.6 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII

Katika sehemu hii tumeangalia yale yaliyoandikwa kuhusiana na yale tunayoyashughulikia. Mulokozi (1976) amechambua maudhui katika kazi za Kezilahabi. Amejadili kwa kifupi maudhui yanayojitokeza katika riwaya ya *Kichwamaji*. Hata hivyo, hajaangalia athari za udhanaishi zinazojitokeza katika kazi hii. Kazi hii imetufaa kwani imetupa mwangaza kuhusiana na maswala muhimu ambayo mwandishi ameshughulikia.

Musau (1985) amemwangalia Kezilahabi kama mwandishi aliyekata tamaa. Katika kazi yake, ameshughulikia riwaya tatu za mwandishi huyu ambazo ni *Rosa Mistika, Dunia Uwanja wa Fujo* na *Kichwamaji*. Ameshughulikia kwa kina maudhui ya kukata tamaa, ili kuonyesha vile mwandishi huyu alivyokata tamaa. Kazi yake imekuwa na manufaa kwetu kwa sababu kupitia kwayo tumemwelewa zaidi mwandishi huyu.

Naye Lugano (1989) ameangalia namna Kezilahabi alivyowachora wahusika wake wa kike. Ingawa kazi yetu ni tofauti na kazi ya Lugano, kazi yake imekuwa na manufaa kwetu kwani imetuwezesha kuelewa mazingira ya kijamii ya jamii hii.

Arege (1998) amechunguza mchango wa Kezilahabi katika ushairi huru. Katika kufanya hivi, ameangalia maudhui yanayojitokeza katika mashairi haya. Vilevile ameangalia maana ya maisha na nafasi ya binadamu duniani kama mojawapo ya maudhui yanayojitokeza. Kazi hii imetufaa katika kuelewa vile mwandishi huyu anavyoyaona maisha.

Mbatiah (1998) ameangalia kazi ainati za Kezilahabi ambapo ameziainisha katika makundi mawili. Kundi la kwanza likiwa na kazi za kipindi cha kwanza ambazo ni *Rosa Mistika, Kichwamaji, Dunia Uwanja wa Fujo* na *Gamba la Nyoka*. Hizi ni kazi za miaka ya sabini. Kundi la pili lina kazi za kipindi cha pili ambazo ni *Nagona* na *Mzingile*. Kazi hizi zimeandikwa katika miaka ya tisini. Kazi hii imetufaa kwa sababu, licha ya kutuwezesha kuielewa zaidi riwaya tunayoishughulikia, imetubainishia falsafa ya mwandishi huyu.

Irungu (1999) ameangalia dhana ya maisha katika Novela mbili za Kezilabahi: *Nagona* na *Mzingile* kupitia kazi hii, tumemwelewa mwandishi huyu zaidi.

Mbatiah (2003) ameifanyia tahakiki riwaya ya *Nguvu ya Sala*. Kazi hii imekuwa na manufaa si haba kwetu kwani imechunguza na kutathmini riwaya hii kwa upande wa fani na yaliyomo. Vilevile kazi ya Magare (2002) imetufaa katika kuyaelewa maswala yanayohusiana na udhanaishi kwa sababu ametumia nadharia ya udhanaishi katika kuiangalia tamthilia ya *Amezidi* kama kazi ya kiubwege.

## 1.7 MSINGI WA KINADHARIA

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya kisosholojia. Nadharia yenyewe iliasisiwa na Mfaransa kwa jina Hippolyte Taine. Huyu aliiona kazi ya fasihi kama picha ya kijiografia, kimazingira na kitamaduni ambamo kazi hiyo imezuka. Alisisitiza kuwepo kwa uhusiano kati ya fasihi na jamii aliposema kuwa ni sharti tuyaelewe mazingira ya kijamii na mtazamo wa kijamii ambamo msanii husika amekulia ili tuweze kuielewa kazi ya sanaa, msanii au kundi la wasanii. Vilevile, alidai kuwa kazi ya fasihi inaweza kuchukuliwa kama rekodi ya kweli ya maisha ya watu. Riwaya, kwa mfano, ni kioo kinachoakisi vipengele vyote vya maisha ya jamii. Aliendeleza madai yake kwa kusema kuwa, kwa vyovyote vile, fasihi haiwezi kutenganishwa na harakati za binadamu ambazo huongoza maisha yake kwani fasihi yoyote ile ni zao la jamii.

Mazingira yamzungukayo msanii humwathiri. Athari hizi hujitokeza katika kazi ya msanii husika. Hili ndilo suala analolisisitiza Gachukia (1980:9) anaposema :

> Mhakiki anapaswa kuelewa na kutambua hali ya mambo na mazingira yanayokuza mwandishi ili kutoa tahakiki halisi na ya kweli. (Tafsiri yetu)

Gachukia anaendelea kusema kuwa hali za kihistoria, kijamii na kisiasa ndizo huchochea ubunifu katika msanii.

Hivyo basi, ni dhahiri kuwa fasihi huumbwa na msanii kutokana na tajriba mbalimbali anazozipata katika mazingira anamojikuta. Ni kwa sababu hii Ngugi wa Thiong'o (1977:xv) anasema :

> Fasihi ni dhihirisho la ujumi na ubunifu wa jamii katika kupigana na mazingira yake ili kuweza kupata mahitaji ya maisha, chakula, mavazi, makazi na katika mchakato huo, kujiumba upya katika historia. (Tafsiri yetu)

Anaendelea kusema kuwa fasihi hupewa umbo, sura na hata mwelekeo wake na msukumo wa kijamii, kisiasa na kiuchumi katika jamii fulani. Hivyo, inabainika kuwa fasihi haiibuki katika ombwe tupu. Ina uhusiano mkubwa na maisha ya jamii kwa jumla. Kwa sababu hii ni wazi kuwa mhakiki hawezi kupuuza swala la mazingira anapohakiki kazi ya msanii.

Nadharia hii inapendekeza kuwa uhakiki wa fasihi uwe sawa na ule wa kisayansi, hivi kwamba, jinsi hali ya hewa inavyolazimu kuwepo kwa aina fulani ya mimea mahali fulani, ndivyo hali ya mazingira iamuavyo kuchipuka kwa aina mbalimbali za sanaa. Kazi za kifasihi basi hazina budi kuhusishwa na mazingira zinamotoka.

Hii ni nadharia ambayo inapinga mitazamo ya nadharia ambazo hushikilia kwamba fasihi 'iko huru' na kwamba haina lazima ya kujihusisha na masuala ya kijamii. Nadharia ya kisosholojia

## TANBIHI

1. Taz. Robert, A (1995) *The Cambridge Dictionary of Philosophy*. U.S.A Cambridge University Press uk 29
2. Heinemann, F. (1958) *Existentialism and the Modern Predicament.* New York Harper & Brothers Publishers. Uk. 56
3. Kama 1 hapo juu uk 812
4. Taz. Wamitila K (2003) *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia* Nairobi Focus Publishers Uk. 248.
5. Foulquie, P ( 1948) *Existentialism* London Dennis Dobson Ltd. Uk 60
6. Warnock, M (1970) *Existentialism* New York Oxford Unversity Press. Uk. 126
7. Taz. Mueller, R (1964) *The Testament of Samwel Beckett.* London Faber and Faber uk. 110
8. Njogu, K na Chimerah R (1999) *Ufundishaji wa fasihi nadharia na mbinu* uk. 14
9. Taz. Mbatiah M (1998) 'Mienendo mipya katika uandishi wa Kezilahabi: *Nagona* na *Mzingile*' katika *Mulika* na 24. TUKI, Uk. 2

huangazia hata vipengele vilivyo nje ya kazi ya sanaa kama vile mazingira ya mwandishi, maisha yake na maisha ya jamii yaliyochangia kuzuka kwa kazi hiyo. Taine alisema kuwa wasanii wanaweza kutofautiana kwa sababu ya kuwa wamezaliwa katika vipindi tofauti, wamekulia katika maeneo tofauti au wametoka katika nchi tofauti. Hivyo, alipendekeza kuwa waangaliwe sambamba na muktadha wa wanakotoka ili waeleweke.

Kwa mkabala huu, tumechunguza mazingira walimoandikia Wamitila na Kezilahabi. Mazingira haya yakiwa ya kiuchumi, kisiasa, na kijamii. Tumechunguza haya ili kuona jinsi ambavyo mtazamo wa kidhanaishi wa kila mwandishi ulivyoathiriwa na mazingira yake. Tumetumia nadharia hii ya Kisosholojia kujaribu kuchunguza ikiwa mazingira ya Kazilahabi na Wamitila ndiyo yaliyochangia katika kuibua viwango tofauti vya udhanaishi katika *Nguvu ya Sala* na *Kichwamaji*.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani. Tulizisoma riwaya tulizoshughulikia kwa undani ili tuweze kuzichanganua. Vile vile tulisoma kazi nyingine ambazo zinahusiana na somo letu la utafiti. Hizi ni pamoja na tasnifu, majarida na makala mbalimbali.

Tulisoma vitabu vinavyoelezea kuhusu nadharia na falsafa ya udhanaishi. Hatukuwa na budi kuzipitia kazi mbalimbali za waandishi kama Kaufmann, Greene, Lepp, Warnock na wengine.

# SURA YA PILI

## ATHARI ZA UDHANAISHI KATIKA *KICHWAMAJI*

## 2.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tumeyajadili maudhui ambayo mwandishi wa *Kichwamaji* ameyashughulikia. Katika kujadili maudhui, athari za udhanaishi ambazo zinajitokeza katika riwaya hii zimebainishwa. Aidha, sura hii inatazama mazingira ambayo yameibusha kazi ambayo ina athari za udhanaishi. Msanii hupata tajiriba yake kutoka kwa jamii anayoiandikia na huchochewa na yale anayoyashuhudia katika jamii yake. Hivyo kazi ya mwandishi inaweza kuonyesha ni mazingira ya aina gani yaliyomzunguka wakati wa kuisanii kazi yake.

## 2.1 MAUDHUI

### 2.1.1 Elimu na Utamaduni

Kezilahabi ameyaangazia maswala ya elimu na utamaduni katika kazi zake nyingi, na hasa katika riwaya ya *Kichwamaji*. Huenda amefanya hivi kwa sababu ya mambo yaliyobainika katika kipindi alichoiandika kazi hii.

Mazingira ya wakati aliyoandika yalishuhudia upapiaji wa Waafrika wa elimu ya kigeni. Kabla ya majilio ya wakoloni, Waafrika walikuwa na elimu yao. Vijana walipokea mafunzo kutoka kwa wazazi. Baada ya kuja kwa wakoloni, mambo yalibadilika kwa sababu elimu ya Magharibi iliyoanzishwa iliwafunza vijana kuwa ni machache mno ambayo wangejifunza kutoka kwa wazazi. Malengo ya elimu ya Magharibi yalikuwa tofauti kabisa na yale ya elimu ya Waafrika.

Elimu ya Waafrika ilikusudia kumtayarisha aliyeipitia ili aweze kufaa jamii kulingana na mazingira na mahitaji mbalimbali. Kwa upande mwingine, wakoloni walikuwa na nia yao. Kama asemavyo Arege (1998:31):

> Elimu hii ililenga katika kuwaondoa Waafrika kutoka katika misingi yao ya kitamaduni ili kufuata na pia kuutumikia utamaduni wa kigeni.

Kezilahabi anatuonyesha kuwa mazingira ya kijamii yalikuwa yamebadilika kwa sababu ya elimu ya kikoloni. Vijana ambao walikuwa wamesoma walikuwa wamekengeuka. Ukengeushi ni mojawapo ya sifa za udhanaishi. Wale waliokengeuka walijitenga na utamaduni wao pamoja na jamii zao. Haya ndiyo anayoelezea Wanjala (1978:20) anaposema kuwa Waafrika waliosoma walihisi kuwa utamaduni wa jamii za Kiafrika kabla ya majilio ya wakoloni umepitwa na wakati.

Kwa kiasi kikubwa, ukengeushi unadhihirika kupitia kwa wahusika Kazimoto na Manase ambao wamesoma hadi chuo kikuu. Kazimoto anapoenda ziwani kumtafuta rafiki yake Kamata, anakutana na wavuvi watano. Hawa hawajasoma sana lakini wanaonekana kuwa na furaha. Ingawa hawa wavuvi ni vijana kama Kazimoto, anaona kuwa elimu yake ndiyo ambayo imemtenganisha na wenzake. Anasema:

> Hapo ndipo nilipoanza kufikiri moyoni kwa nini nilisoma mpaka chuo kikuu.... Niliwaonea wivu wenzangu ambao tuliachana darasa la nne. Wao sasa walikuwa wakicheza zeze na kupiga vishindo kwa furaha. Niliona kwamba elimu ilikuwa sumu ya furaha yangu (uk. 50)

Ni wazi kuwa wale waliosoma waliona kwa jicho tofauti na wasiosoma. Matusi kwa wavuvi ni njia ya kujifurahisha lakini kwa Kamata ni dhambi. Kucheza zeze na kupiga vishindo ni mambo ya maana kwa wavuvi. Kwa Kazimoto, kusoma vitabu na magazeti ndilo jambo la maana. Hivyo Kazimoto anaona vigumu kujitambulisha na hao wenzake. Anajutia masomo yake. Wanjala (1980:15) anatilia hoja hii uzito anaposema :

> Mwafrika aliyesoma aliona vigumu kuhifadhi miiko

> na ibada zilizowaunganisha watu wake pamoja.
> Alitenganishwa na sherehe za kuimba na kupiga ngoma.

Aidha, mjadala kati ya Matilda, Kazimoto na vijana wengine unatuelekeza kuhisi kuwa elimu imeleta ukengeushi. Kijana mmoja ana wazo kuwa tabia ya vijana ya kuwadharau wazazi inatokana na elimu. Asema, "dharau hii imeletwa na elimu". Wanafikiri kwamba mawazo yote ya wazee ni ya kijadi. Jamii ya Waafrika iliwafunza watoto kuwaheshimu wazazi. Yeyote ambaye aliwadharau alikuwa akifanya kinyume na matarajio, na hivyo angesemekana kuwa amekengeuka. Inavunja moyo kuona kwamba elimu ya Magharibi haikuimarisha maadili katika jamii. Badala yake, inawatenganisha wanajamii.

Fikra za Manase kuhusu muziki wa Kiafrika zinatupa picha nzuri ya ukengeushi. Kazimoto anapomwambia aweke rekodi ya Kongo au Afrika Mashariki, Manase anajibu kuwa hakuwa na hata moja. Kwa dharau anamuuliza Kazimoto:

> Hivi muziki wa Kiafrika unakupendeza nini? Unalia mbu!
> mbu!mbu! Tangu mwanzo mpaka mwisho, mwishowe
> unaleta mbu ndani ya nyumba (uk.133)

Dondoo hili ni ithibati kuwa Manase amejiweka mbali kabisa na utamaduni wake. Anaudhihaki muziki huu na kuuona kama ambao hauna manufaa yoyote. Kwake muziki wa Kizungu ndio bora. Anautolea sifa kemkem ambazo zinaonyesha jinsi anavyohusudu muziki huo. Anasema:

> Muziki wa Kizungu wa mapenzi ukilia unaweza kuona picha ya watu wakipendana...unafurahisha moyo na mwili mzima hata wewe unajiona hukanyangi chini (uk.133).

Mojawapo ya dhima za muziki ni kuburudisha. Kulingana na Manase, muziki wa Kizungu ndio unaomgusa na kumburudisha msikilizaji. Anakiri kuwa anamkumbuka bibi yake kupitia nyimbo za Kizungu. Mandhari kwenye nyumba ya Manase yanashadidia athari ya ukengeushi

ıaishani.mwa Manase. Mandhari yenyewe, kama tunavyoelezwa na Kazimoto, ni ya Kizungu. ınasema:

> Mambo niliyoyaona humo chumbani yalikuwa kama haya. Radiogramu kubwa kama meza, makochi na meza katikati iliyokuwa imepambwa na kitambaa cheupe...ubao wa chess...sakafu nyekundu. Kuta zilikuwa na miigizo ya picha zile zilizochorwa na kina Raphael na Michelangelo (uk.132).

ʒi wale tu waliofika vyuo vikuu ambao wamekengeuka. Hata wale wenye elimu ya wastani ːama Salima wameathirika. Mpishi aliyeajiriwa anapochelewa, Salima anamkaripia. Ingawa ımri wa mpishi unastahili heshima, anakaripiwa kama mtoto mdogo. Anaomba msamaha na ːueleza sababu yake ya kuchelewa. Haya yote hayamridhishi Salima. Maneno yake kwa mpishi ˈmzee) yanaonyesha sio tu utovu wa heshima bali hata ukatili. Anamwambia:

> Hadithi ya mkeo haituhusu sisi...umechelewa karibu saa mbili nzima. Utakatwa mshahara. Mwezi huu umevunja karibu glasi tatu, hizo pia zitakatwa (uk.135).

Kwamba bibi wa mpishi alikuwa mgonjwa sana, hakumfanyi Salima amhurumie mpishi wake. Baada ya kumkemea anampa maagizo kisha anarudi kukaa na kina Kazimoto. Yale yanayotukia hapa yanatukumbusha enzi za wakoloni ambapo Wazungu waliwaajiri Waafrika kama wapishi. Wake wa wazungu hawakufanya kazi ya jikoni. Waliagiza tu, kama afanyavyo Salima.

Waaidha, kuna kutoelewana kati ya vijana na wazee. Bonde lililoko kati ya makundi haya mawili ni kubwa. Bonde hili limesababishwa na mabadiliko katika jamii ambapo vijana waliosoma ndio wenye vyeo na hivyo mishahara mikubwa. Waliosoma (vijana) wana uwezo wa kuwaajiri wasiosoma (wazee) kama wapishi. Kwa sababu hii, waajiri wanahisi kuwa wanastahili kuheshimiwa na waajiriwa. Utamaduni wa Kiafrika unaosisitiza heshima kwa wazee sababu ya umri hauna mashiko tena. Kazimoto anasema:

> Nilikaa kimya nikitazama kizazi kipya kikigombana na babu zake. Kwa mara ya pili niliona wazee wetu wanatukimbia. Nilijiuliza kama hatuna lo lote la kutegemea kutoka kwa wazee wetu isipokuwa kuwafanya wapishi, kuwakanyanga, kuwatisha na kuwakaripia (uk.134).

Kezilahabi anaonyesha kuwa elimu ya kikoloni iliwatenganisha wazee na vizazi vilivyofuata. Kwa vijana, wazee hawakuwa na nafasi katika ulimwengu uliojaa elimu na utamaduni wa kigeni. Tunashuhudia ukweli huu wakati Manase anamfukuza mzee kutoka afisini mwake, eti kwa sababu ameingia na fimbo. Ndiposa Kazimoto anasema kuwa mzee alipotoka nje, aliona (Kazimoto) wazee wakiwakimbia vijana na uhusiano kati yao ukikatika. "Niliona wazazi wakiwakimbia watoto wao ambao sasa walikuwa wakali kama simba" (uk.7). Vijana ndio wanasababisha utengano huu. Mwandishi anatumia tashbihi kuonyesha ukali wa kizazi kipya (vijana) kwa wazee. Mwandishi amekerwa na mambo haya na kwa kupitia kwa Kazimoto anasema:

> Moyo wangu ulivurugika kwa mchanganyiko wa hasira na huzuni nilipoona mzee akikimbia serikali yake (uk.7)

Ni wazi kuwa Kezilahabi amekatishwa tamaa na ukweli kuwa wasomi waliokengeushwa na elimu ya Magharibi kama vile Kazimoto na Manase hawawezi kuwa ruwaza ya kuigwa katika jamii. Yale wanayotenda ni mambo yanayoudhi. Manase anamnajisi Rukia na kumtia mimba iliyosababisha kifo chake wakati anapojifungua. Kama Mkuu wa Wilaya, Manase anakosa uwajibikaji. Kazimoto naye ana tabia mbaya ya uzinzi na wanaojaribu kumuiga kama vile Kalia wanaishia katika maangamizi. Kalia aliuawa kwa sababu ya kuwabaka wanawake.

Mwandishi ametamauka kwa kuona kuwa wasomi ambao wangeleta maendeleo katika jamii na hivyo kuinua hali ya maisha wanaipeleka jamii yao katika maafa. Kizazi cha vichwamaji – watoto ambao wanazaliwa na vichwa vikubwa – kimetokana na wasomi. Linalovunja moyo zaidi ni ukweli kuwa hakuna matumaini ya kuutibu ugonjwa unaosababisha watoto kuzaliwa wakiwa na vichwa vikubwa.

Kezilahabi anaonyesha kuwa elimu ya Magharibi iliyopuuza utamaduni wa Mwafrika na kumkengeusha inakatisha tamaa; sawa na falsafa ya udhanaishi ambayo inatamausha.

### 2.1.2 Mapenzi na Ndoa

Ndoa ni sehemu muhimu ya maisha ya binadamu. Mwandishi ameshughulikia maudhui ya mapenzi na ndoa kwa mapana. Kupitia maudhui haya, mwandishi ameonyesha kwamba maisha ya binadamu yamekumbwa na matatizo katika takriban nyanja zote. Hata asasi kama ndoa ambayo inatarajiwa kuleta furaha katika maisha imekosa furaha. Hii ni athari ya udhanaishi. Wanaudhanaishi wana maoni kuwa maisha ya binadamu ambayo yametawaliwa na udhia hayawezi kuwa na furaha kamwe. Katika jamii za Kiafrika, asasi ya ndoa ilithaminiwa sana. Mbiti (1990:104) anaeleza kuwa ndoa iliangaliwa kama jukumu takatifu ambalo kila mtu alitarajiwa kulitekeleza. Asasi hii ilikuwa muhimu kwa vile ilikuwa njia ya kuendeleza jamii - watoto walizaliwa katika mazingira ya ndoa. Mapenzi yalihusishwa na ndoa na ilikuwa ni hatia kujiingiza katika ngono kabla ya ndoa. Kama asemavyo Philips (1953:47):

> Wasichana walikumbushwa umuhimu wa kuwa bikira kabla ya ndoa. Aidha waliambiwa kuwa wangetia aila yao aibu endapo hawakuwa wamejitunza (tafsiri yetu)

Kuoa zaidi ya bibi mmoja kulikubaliwa. Hata hivyo, uaminifu katika ndoa ulisisitizwa. Mbiti (1990:146) anasema :

> Kufanya mapenzi katika jamii ya Kiafrika hakukuhusishwa na sababu za kibayolojia tu. Kulikuwa na manufaa ya kidini na kijamii pia. Manufaa haya yalishikiliwa kuwa takatifu na kuheshimiwa. Kutozingatia hayo kuliandamana na hatua madhubuti (tafsiri yetu)

Hata hivyo, Kezilahabi anatuchorea picha tofauti kuhusu suala la mapenzi na ndoa. Hii ni ishara kuwa jamii yake ilikuwa imepitia mabadiliko. Mapenzi nje ya ndoa ni kama jambo la kawaida tu. Kazimoto ambaye ni kijana wa chuo kikuu ana uhusiano wa kimapenzi na Vumilia. Vilevile analala na Sabina kabla ya ndoa yao. Aidha, anahusiana na Pili na Nyabuso. Ubikira umekosa maana katika jamii hii. Yule ambaye anajaribu kujitunza hathaminiwi. Wavulana wengi wanamtoroka Sabina kwa sababu hataki kujihusisha na mapenzi kabla ya ndoa. Tunaelezwa haya kuhusu Sabina, "ule muujiza wa kupata mchumba anayeridhishwa na maneno tu alikuwa bado kuuona."

Mwishowe Sabina analazimika kuvunja kanuni zake anapoona matumaini ya kuolewa yanafifia. Analala na Kazimoto kwa matumaini kuwa atamuoa. Anasema:

> Kazimoto; alisema pole pole, ninafanya hivi kwa sababu
> ninaamini kwamba huenda siku moja tukaoana (uk.50).

Wasichana wengi wanapata mimba wakiwa hawajaolewa na jambo hili halielekei kuwasumbua. Ni kama kwamba limeshakubalika katika jamii. Kazimoto haelewi kwa nini Rukia anasikitishwa na mimba ilhali wasichana wengine wanaoipata wanacheka na kufurahi kama kawaida" (uk 74). Naye Kabenga asema kuwa, "dansi ya kushikana wawili wawili ilipoingia nchini usafi ukaisha". Usafi hapo ni ubikira. Inavunja moyo kuona kuwa maadili kama vile kujiepusha na uzinzi ni mambo ambayo yamekosa maana.

Ni jambo la kusikitisha kuona kuwa ndoa haiheshimiwi. Kabenga, ambaye ameoa ana jicho la nje. Anaenda kulala kwa Tegemea, mwanamke ambaye alikuwa kahaba. Nao wanaume ambao walikuwa wameoa walikuwa wakitembea na wanawake wengine. Kwa mfano, tunaambiwa kuwa Nyabuso (mwanamke huyu hakuwa ameolewa) aliweza kumfuata mume nyumbani na kumwita 'bwanangu' mbele ya mke wake halali (uk 69).

Aidha, vijana wanatongoza wanawake ambao wameolewa. Matilda ni mmoja wa anayetongozwa lakini anakataa. Kazimoto anakiri kuwa alizoea kuzini na Pili kabla na baada ya ndoa.

Ule umuhimu na uzito ulioambatanishwa na asasi ya ndoa unaelekea kufifia. Katika mjadala kati ya Kazimoto na Manase kuhusu chanzo cha vijana wadogo kushiriki ngono na kutiana mimba, tunaelewa kuwa ndoa imepoteza umuhimu wake kinyume na awali. Manase anasema:

> Zamani, jambo la maana ambalo kila mwanadamu alikuwa akitegemea maishani lilikuwa ndoa. Lakini siku hizi mambo kama elimu na pesa yamezuka na ndoa imekuwa kama kitu kisicho na thamani (uk 144)

Dondoo hili laonyesha kuwa nafasi ya ndoa imechukuliwa na elimu na pesa. Ni wazi kuwa jamii inayozungumziwa na mwandishi imepetia mabadiliko ya kijamii na kiuchumi. Elimu rasmi ambayo ilichukua miaka mingi, imechukua mahala pa mafunzo ambayo vijana walipata kutoka kwa wazazi. Kwa mujibu wa Manase:

> Vijana wako tayari kuahirisha ndoa, lakini wasome, ingawa wana umri wa miaka thelathini au zaidi (uk. 144).

Ingawa Kezilahabi aliandika kazi yake baada ya Azimio la Arusha (1967) ambalo lilikuwa mwanzo wa siasa mpya ya Ujamaa, masalia ya Ubepari bado yako. Ubepari huthamini pesa sana. Wasiokuwa nazo hufanya juu chini kuzitafuta. Kuna wengine ambao wanavunja maadili mradi tu wapate pesa. Tegemea ni mfano bora. Hajali kulala na Kalia, mvulana mdogo, bora tu ampatie pesa. Hata Kalia anapomwambia vile alivyopigwa na babake alipoiba pesa ili amletee, Tegemea anamwambia kuwa hayo ndiyo mapenzi halisi.

Pili mwanamke kiberenge anamwandikia Kazimoto barua kumshukuru kwa pesa alizompa. Nyabuso anawalisha wazazi wake kwa pesa azipatazo kutoka kwa wanaume mbalimbali. Aidha, tunamwona Kabenga akimlalamikia kimada wake Tegemea kuwa ana tamaa nyingi ya pesa; na kwamba hawezi kumpenda mtu bila pesa. Ama kwa kweli pesa zimechukua nafasi ya mapenzi ambayo ni msingi katika ndoa. Mwandishi anaonyesha kuwa asasi hii imekumbwa na matatizo si haba. Kwanza, kuna wazazi ambao hawataki mtoto wao aoe ama aolewe na jamaa fulani. Hii

ndiyo sababu wazazi wa Matilda wanamwitisha Kamata mahari nyingi ili akate tamaa na amwache.

Ndoa nyingi hasa za wasomi zimekumbwa na matatizo; hivyo hazina furaha. Sabina, ambaye ameolewa na Kazimoto anahuzunika sana anapotambua kuwa bwanake ana uhusiano na mwanamke mwingine. Ndoa hii vilevile inakumbwa na msiba wa kupoteza mtoto. Msiba huu unasababishwa na Kazimoto ambaye alizini na Pili. Matarajio ya wahusika katika ndoa hii kuwa wazazi hayakufikiwa. Mfano mwingine ni ndoa kati ya Manase na Salima. Hawa pia hawana furaha hata chembe hasa baada ya kupata mtoto mwenye kichwa kikubwa.

Mandhari nyumbani kwa Manase yanaonyesha ukosefu wa furaha. Kila kiumbe katika makazi hayo kinatangaza huzuni. Ndege anataka kuimba wimbo wa huzuni, paka analia kwa huzuni. Sauti fulani ya huzuni inasikika katika mlio wa viatu vya Salima na hata macho yake hayaonyeshi furaha kamwe. Uso wa Manase vilevile unaonyesha huzuni (uk. 205). Mtoto aliyezaliwa katika ndoa hii ni ishara ya huzuni.Mtoto huyo alikuwa wa kushangaza kwa sababu kichwa chake kilikuwa na ukubwa usio wa kawaida. Salima anakasirika sana Kazimoto anapoulizia kuhusu mtoto huyu. Pengine mtoto anamkumbusha tabia ya uzinzi ya bwanake. Kupitia kwa ndoa hii, Kezilahabi anatoa rai kuwa maisha ya binadamu yametawaliwa na huzuni. Furaha imekosekana hata katika asasi ambayo inatarajiwa kuleta furaha. Ikiwa maisha yamejaa huzuni, basi yana maana gani?
Hoja hii inatiliwa nguvu na Senkoro (1982:89) anaposema haya:

> Maisha kwa kufuatana na Euphrase Kezilahabi hayana maana kwani ni tanzia tupu.

Kezilahabi anayaona maisha kupitia kwa jicho sawa na wadhanaishi. Kwao maisha hayana maana.

Aidha, kuna ukengeushi katika ndoa. Sabina analalamika kuwa bwanake hamwiti jina la Kizungu. Baada ya kufikiria sana, Kazimoto anaamua kumwita Hani. Hani ni jina ambalo limetoholewa kutoka kwa neno la Kiingereza 'Honey'. Sabina anapendezwa sana na jambo hilo,

na anaamua kumwita bwanake Hazz (Husband). Kwake kuitana majina kama haya ni ustaarabu. Hathamini majina ya Kiafrika. Amekengeuka. Hata Salima naye ni vilevile. Haoni haya kumsomea mpishi ambaye ni mzee. Naye Manase anamfikiria bibi yake kupitia nyimbo za Kizungu. Hizi zote ni dalili za kukengeuka.

Mwandishi huyu anaonyesha kuwa asasi ya ndoa imekumbwa na matatizo si haba. Hakuna uaminifu. Kuna misiba ya kuwapoteza watoto na hivyo kufanya matarajio ya wazazi kudidimia. Aidha, kupata watoto wasio wa kawaida kunawafanya wazazi wakose furaha. Matatizo haya yote yanayafanya maisha kuonekana magumu na yenye kutamausha.

### 2.1.3 Maisha na Kifo

Kwa mujibu wa wanaudhanaishi, maisha na kifo haviwezi kutenganishwa. Kifo ni kama tukio la mwisho katika kutimiliza maisha. Sehemu hii inaangalia mwandishi alivyoshughulikia maswala haya.

Kuhusu maisha, Kezilahabi anatoa rai kuwa maisha ni adhabu kubwa. Adhabu daima huhusishwa na uchungu pamoja na mateso. Mwandishi anatumia istiari hiyo – maisha ni adhabu kubwa – kutufanya tuhisi kuwa maisha ni magumu na yamejaa dhiki. Ili kuonyesha vile maisha yalivyo adhabu kwa mwanadamu, anatoa mfano wa mtu ambaye aliamrishwa kujaza maji ndani ya pakacha. Hili ni jambo amablo linasumbua na haliwezekani. Kazimoto anasema :

> Niliona adhabu kubwa ya mwanadamu ni maisha
> yenyewe… Maisha ambayo hayashibishwi wala
> kuridhishwa (uk.94)

Mwandishi huyu vilevile ametumia sitiari ya dunia kama sahani yenye joto kali ili kuuweka ujumbe wake wazi. Katika shairi lake la 'Mto Nili' (Kichomi 1974:7) anasema:

> Ni adhabu ya kutosha kupaswa kuishi juu ya sahani yenye
> joto kali ya kukaangia na yaliyopita, yamepita.

Kwake, kuishi tu ni adhabu tosha kwani ni sawa na kuwekelewa kwenye kikaango ambacho kina joto kali. Maisha kama hayo bila shaka ni magumu na hayaridhishi.

Maisha haya ambayo hayaridhishi yanakosa furaha. Ingawa binadamu amejaribu mambo mengi kama vile kuvuta sigara na kucheza ngoma ili ajipatie furaha, yote haya yameambulia patupu. Tunaelezwa:

> Yote mwanadamu wenye akili anafanya kwa jina ambalo limempumbaza akili. Jina 'Furaha' ambalo ni neno jingine la adhabu (uk.94)

Aidha, mwandishi anazua hoja kuhusu maisha kupitia kwa sanamu. Manase anapomweleza Kazimoto kuhusu sanamu iliyo nyumbani kwake, anasema kuwa, "...inatueleza taabu za bianadamu hapa duniani." (uk.206)

Maisha ya binadamu basi yanaonekana kutawaliwa na madhila. Mawazo haya yanaoana na yale ya wadhanaishi wanaoshikilia kuwa binadamu ni kiumbe pweke aliyetupwa katika ulimwengu unaomtesa. Ni kupitia kwa sanamu pia ambapo tunapata hoja kuwa maisha hayana thamani. Mwisho wa binadamu ni kaburini ambapo anacheka na sisimizi – wadudu wadogo sana. Tunajiuliza tofauti ya binadamu na sisimizi ni ipi? Kupitia kwa Kazimoto, mwandishi anayalinganisha maisha na maji yateremkayo huku yakikusanya takataka. Anasema:

> .... Na kama maji ya mto yakusanyavyo takataka za kila aina ndivyo mwanadamu akusanyavyo taka wakati wa maisha yake (uk.102).

Hapa mwandishi ametumia takataka kuashiria shida anazokumbana nazo mwanadamu. Iwapo kile ambacho binadamu anafanikiwa kufanya miashani ni kujilimbikizia taabu, basi kweli maisha hayo hayana maana. Ni kwa sababu hii ambapo Kazimoto anaona kuwa ulimwengu si pahali pazuri pa kuishi na anashangaa kwa nini maisha hayachukuliwi mapema. Maneno haya ni ya mtu ambaye haoni haja ya kuishi. Amekata tamaa.

Maisha yanaonekana kuwa fumbo – hayaeleweki. Haya ndiyo Kazimoto anatilia nguvu anaposema:

> Mara zingine, ninaona kurukaruka ndiyo kazi tu imebaki kwa mwanadamu ili kuondoa ile hali yake ya kushindwa kuelewa fumbo la maisha... (uk.134).

Kupitia kwa picha yenye mistari iliyokuwa na Manase, tunafahamu namna mwanadamu alivyonaswa kwenye mtego wa maisha na hana njia ya kujisalimisha. Tashbihi inayomfananisha mwanadamu na samaki inaonyesha wazi namna mja hana uwezo juu ya maisha yake. Nayo ngozi ya simba, kama anavyoelezea Manase, ni ya kumfanya mtu atafakari juu ya maisha. Kwa kuiona tu ngozi hiyo, mtu anapatwa na woga unaomzuia kuona chochote isipokuwa kukosa maana kwa maisha. Manase anakiri:

> ... Watu wanaoishi ndani ya nyumba hii hawaoni tena maana ya maisha (uk.209)

Watu wanaorejelewa na dondoo hili ni Manase na bibiye Salima. Wametamauka. Kazimoto vilevile amekata tamaa maishani. Ndiposa anasema kuwa wazo la Manase kuhusu maisha lilikuwa kama lake - maisha hayana maana. Kama vile mwalimu atumiavyo vifaa vya kufundishia kuweka wazo wazi kwa wanafunzi wake, mwandishi anatumia kinyago, ngozi za simba pamoja na picha kufafanua wazi namna maisha ni magumu, ya kutisha na yenye kukatisha tamaa. Kutumiwa kwa vifaa hivi kunatufanya tuhisi uduni wa maisha.

Aidha, kuna wazo kuwa maisha ya binadamu ni mafupi. Vifo vingi vinavyotokea vinaashiria ukweli huu. Rukia, dadake Kazimoto anaaga huku akijifungua. Huyu alikuwa msichana mdogo. Kifo chake vilevile kinaonyesha matamanio yasiyofikiwa. Rukia alitaraji sana kumsaidia mamake. Anasema:

> Mama, hufahamu masikitiko yangu. Nilitegemea sana kukusaidia lakini sasa siwezi (uk.74)

Kalia, kakake Kazimoto, anauawa angali kijana mdogo kutokana na tabia yake ya kuwanajisi wanawake. Kifo chake kinatukumbusha ufupi wa maisha na wakati huo huo kutuonyesha namna uchaguzi afanyao mwanadamu unavyoweza kuwa na madhara. Anapoamua kuwa mbakaji, Kalia anauawa na mwili wake unatupwa mtoni.

Aidha, kuna kifo cha mama Rukia, kifo cha Kazimoto, mtoto wa Kazimoto na mwendeshaji baiskeli. Tuza anapotembelea bintiye anamweleza Kazimoto vile wazee wengi wamefariki. Anatumia tashbihi, 'wanapasuka kama kuni', kuonyesha vile wanafariki upesi. Vifo hivi vinaashiria kuwa maisha ulimwenguni hayadumu. Kifo hakibagui. Mtu anaweza kufa akiwa mtoto, kijana au mzee. Kifo kama vile maisha, ni fumbo ambalo halijang'amuliwa. Binadamu yeyote anayejaribu kufikiria kuhusu kifo huwa anajisumbua na kujikosesha raha kama aelezavyo Manase:

> … Mtu asiye na raha hapa duniani ni yule ajaribuye kufahamu… kwa nini atakufa. Katika maisha yake yote, jambo la kifo litakuwa linamsumbua bure (uk. 137)

Waaidha,hakuna mpaka bayana kati ya kuishi na kufa.Kama asemavyo Manase, kufa ni kuishi (uk. 206). Ikiwa mwanadamu aliye hai ni sawa na maiti, kuna haja gani ya mtu kuishi huku akiteseka? Maisha hayana umuhimu wowote. Wazo hili linatiliwa mkazo na Manase anapomweleza Kazimoto juu ya sanamu.
Anamwambia:

> Ukifikiri zaidi utaona kuwa inaonyesha picha nzuri ya maisha yetu… ukweli ni kwamba sisi wanadamu tunakufa polepole…Tangu mwanadamu anapozaliwa anaanza kufa polepole ingawa yeye anajiona yu sawa. Siku zake zinakatika moja moja. Kaburi ni hatua ya mwisho tu (uk.206)

Kifo ni sehemu ya maisha na ni lazima kila mtu afe. Hata hivyo, mwanadamu hajakubali ukweli huo. Mtu afapo, waliobaki husikitika sana na kuomboleza. Mwandishi anawashauri waliobaki kusahau msiba na kuendelea na maisha yao. Baada ya kifo cha Rukia na mamake, Kazimoto ananunuliwa pombe na wanakijiji ili asahau msiba. Aidha, shairi 'Nenda Ukanywe' katika *Kichomi* (1974) linatukumbusha kuwa hakuna haja ya kusikitika kwani hata tufanye nini aliyeaga hawezi kufufuka.

> Nenda ukanywe!
> Kwani
> Nani alikula asile tena!
> Nani aliruka hewani asitue?
> Lakini nani alikufa akarudi? (uk.30)

Katika dondoo hili, tunaona kuwa Kezilahabi ana mawazo sawa na waandishi wengine wa kidhanaishi kama vile Samuel Beckett. Wote wanaona kuwa kifo ni tukio la mwisho katika maisha ya binadamu. Katika diwani ya *Kichomi* (1974:30), Kezilahabi anatumia shairi 'Nenda Ukanywe' kuonyesha hatua za maisha ya binadamu.

Binadamu afikiriapo kuhusu swala la kifo hana budi kutamauka kwa sababu huona kuwa juhudi zake zote maishani huishia kaburini. Kama mojawapo ya teneti za udhanaishi inavyodai, malengo ya mwanadamu huwa hayana maana yoyote binadamu afapo. Hii ndiyo sababu mwandishi anatoa rai kuwa maisha hayana maana na ni heri kufa mtu akiwa mchanga. Kazimoto, baada ya kufikiria juu ya maisha anasema, "Niliona heri ningekufa ningali mtoto" (uk.102).

Yote haya, yanatuelekeza katika kutambua ufupi, utupu, na uduni wa maisha ya binadamu. Ikiwa juhudi zote maishani lazima zifukiwe kwenye kaburi, basi maisha yenyewe yana thamani ipi? Anayeishi anapata faida gani? Haya ni baadhi ya maswali ambayo wadhanaishi hujiuliza. Kwa kuwa maisha yamejaa dhiki, wadhanaishi huona kuwa kifo kinampumzisha mja kutokana na taabu za ulimwengu.

Kazimoto anapotambua kuwa maisha yake yametawaliwa na huzuni kwa sababu ugonjwa alioupata na kumwambukiza mkewe haungetibika, anaamua kujitia kitanzi. Kifo hakiwezi kuwa suluhisho la matatizo ya maisha kama asemavyo Musau (1985: 48):

> Kifo ni suluhisho la wadhanaishi ambao hufikiria kwamba
> kinaweza kuleta maana katika maisha yasiyo ya maana.

Kezilahabi anaonekana kuafikiana na wadhanaishi kwa jinsi anavyowaua wahusika wake. Rosa Mistika, mhusika mkuu katika riwaya ya *Rosa Mistika* anajiua baada ya kukataliwa na mchumba wake. Hili ni suluhisho la waliokata tamaa maishani. Mwandishi amechukua mtazamo unaooana na wadhanaishi kama vile Albert Camus ambaye amedai kuwa, kifo kinaweza kuleta maana katika maisha katili yasiyo na maana. Inatamausha kufahamu kuwa binadamu hana uwezo juu ya kifo.

### 2.1.4 Dini

Udhanaishi hujishughulisha na swala la Mungu. Kwa mujibu wa wadhanaishi, ni vigumu kuyakinisha kuweko au kutokuweko kwa Mungu kwa sababu maarifa aliyo nayo binadamu yana kikomo.

Kezilahabi anaonyesha kuwa kuna wanaoamini kuwa Mungu yuko na wakati huo huo kuna wale ambao hawana imani katika Mungu. Mgawanyiko huu wa dhana inayohusiana na Mungu inajitokeza wazi kupitia kwa usemi wa Kazimoto kwamba:

> Mwanadamu atasali, wakati huo huo wengine wanapiga
> kelele kwamba hakuna Mungu (uk.140)

Hata hivyo, kupitia kwa Kazimoto na Manase, mwandishi anadadisi kuwako kwa Mungu. Kinyume na Wakristo ambao huamini kuwa Biblia ni neno la Mungu, Kazimoto anaona kuwa Biblia ni kitabu cha zamani ambacho labda kimepitwa na wakati. Anasema, "Nilianza kujiuliza

kwa nini nilisoma kile kitabu cha zamani – Biblia" (uk.50). Aidha, anatoa maoni yake kwa wazee kuwa anashuku kuwepo kwa Mungu. Anasema, "huenda hakuna Mungu.' (uk 59).

Kutilia shaka kuwepo kwa Mungu kunaendelezwa na ndoto ya Kalia. Kalia anaota akiwa mbinguni lakini haoni Mungu wala watu waliokuwa motoni. Jambo hili linatuonyesha kuwa dhana ya peponi au jehanamu haina mashiko. Hoja hii inatiliwa mkazo na Kazimoto ambaye anashuku kuwepo kwa jehanamu anaposema:

> Shetani naye ana bahati nzuri, kwani.... ninafikiri kwamba wanawake wazuri wengi huenda motoni – kama kuna moto na shetani huwafaidi (uk.114).

Wazo hili linaendelezwa na Kezilahabi katika riwaya yake ya *Rosa Mistika* (1971:59) kupitia kwa mhusika Rosa. Anamwambia padre, "wokovu maana yake nini? Wokovu, wokovu gani! Kama kuna moto basi nitakwenda."

Dhana ya pepo (mbingu) na jehanamu (motoni) huenda sambamba. Ni vigumu kuamini kuwepo kwa jehanamu bila kuamini kuwepo kwa pepo.

Wakristo huhusisha mbingu na Mungu. Wanaamini kuwa Mungu ana makao yake huko mbinguni. Kazimoto ana maoni tofauti. Kwake, wazo la mbinguni limebuniwa tu na mwanadamu aliyeshindwa kupata furaha. Mawazo yake ni ya kudadisi kuwepo kwa Mungu. Anakiri kuwa anaona vigumu kuamini kuwa mbingu ipo. Anapigia mwangwi mawazo ya wadhanaishi kuwa furaha ni kitu ambacho hakiwezi kupatikana humu duniani. Anasema:

> Mwanadamu ni kiumbe ambaye amejaribu kutafuta njia nyingi za kupata furaha. Kwa kuwa ameshindwa kupata furaha hapa duniani, amejenga kichwani mwake kitu kama mbingu, yaani mahali anapotegemea kupata furaha baada ya kufa (uk.137).

Nukuu hii inaonyesha kwamba ni vigumu kwa binadamu kupata furaha humu duniani. Ni kwa sababu hii ambapo amejenga imani kichwani mwake kuwa furaha itapatikana mbinguni. Wakristo huamini kuwa furaha itapatikana huko paradiso baada ya Mkristo kufariki. Mawazo haya yanaelekea kuwa sawa na ya Albert Camus anayedai kuwa furaha ya kudumu haiwezi kupatikana katika maisha ya binadamu (Cruickshank 1958:27).

Ni wazi kuwa mwandishi huyu anaeleza msimano wake kuhusu dini kupitia kwa Kazimoto. Baada ya mtoto aliyezaliwa kuaga, Kazimoto anadadisi kuwepo kwa Mungu. Anashangaa kwa nini Mungu anawadhulumu kwa kuwanyang'anya mtoto wao, ikiwa kweli yupo. Tunasoma:

> Nilianza tena kufikiri juu ya Mungu. Kama kweli Mungu
> Alikuwapo, sikuona kwa nini aliweza kufanya ukatili
> mkubwa kama huo (uk.20).

Kiudhanaishi, wazo la Mungu humjia binadamu baada ya kushindwa kukabiliana na maisha yake. Kulingana na Wamitila (2003:248), kazi mbalimbali za Kierkegaard na hasa *The Concept of Dread, Fear of Trembling* na *Sickness unto Death,* zinaeleza kuwa mwanadamu hupata kimbilio kutokana na mivutano ya maisha kupitia kwa Mungu.

Wazo la dini kama kimbilio la matatizo ya maisha linapatikana baada ya kifo cha mtoto wa Sabina na Kazimoto. Kazimoto anapokiri kuwa amekata tamaa ya kuishi na kupata watoto, Sabina anamkumbusha kuwa Mungu anafahamu kila kitu na kwamba amewawekea kitu kizuri zaidi. Anajifariji na kujipa matumaini kupitia kwa wazo la Mungu. Vilevile mwanadamu anaonekana kulikabili tatizo la woga linalomkabili maishani kupitia kwa dini. Kwa mujibu wa wadhanaishi, maisha ya binadamu hutawaliwa na hofu kuu. Huenda mwanadamu anajitia ujasiri kwa kufikiria kuwa kuna nguvu zinazoweza kumsaidia – Mungu. Ndiposa Kazimoto anasema:

> … Mwanadamu ameamua kwamba kuna Mungu kwa
> ababu ya hali yake ya woga iletwayo na milango ya fahamu (uk.138)

Aidha, swala la Mungu linatatanisha kwani kufikia uamuzi wa kuwepo kwake au la ni vigumu. Kama aulizavyo Pascal Blaise, "tunawezaje kuamua ikiwa Mungu anaishi au haishi? Hili ni kama fumbo kwa mwanadamu." Manase anakiri kuwa haelewi mambo ya dini. Anasema:

> Mimi siku hizi mambo ya dini nimeacha kuyafikiria sana...
> Haifai kujaribu kufahamu mambo usioweza kuelewa (uk.137).

Kazimoto anapojaribu kufikiria kuhusu Mungu, anaumwa na kichwa sana. Huu ni wakati ambapo anamwokoa nyuki kutoka kwa maji. Kwa kitendo chake cha uokoaji, anajihisi kuwa sawa na Mungu. Anaona kuwa Mungu ni kama nguvu zimsadiazo binadamu wakati wa shida. Anapoendelea kutafakari, anaona hata wakati unaweza kuwa Mungu. Anasema:

> Labda tunaweza kusema kwamba ni wakati. Wakati wenyewe ndio Mungu maana haukuumbwa (uk.89)

Ni wazi kuwa swala la Mungu linabaki kuwa kitendawili kwa binadamu mwenye maarifa yaliyo na kikomo. Huu ni udhanaishi.

### 2.1.5 Maisha ya Vijijini na Mijini

Tunapomulika maudhui haya, tunapata kuwa kuna athari nyingi za udhanaishi ambazo zinajitokeza. Kwanza, hali ya maisha vijijini haielekei kuwa shwari. Ingawa Kezilahabi aliandika kazi tunayoishughulikia miaka saba baada ya Azimio la Arusha, malengo ya Azimio hili hayaonekani kufikiwa kikamilifu. Baadhi ya malengo ya Azimio la Arusha yalikuwa kuwaunganisha watu ili wafanye kazi pamoja, wapige vita umaskini na dhuluma na waweze kujitegemea. Pia, viongozi walitazamiwa kujitolea mhanga katika huduma zao kwa taifa. Yale ambayo tunashuhudia kupitia kwa maisha ya vijijini na mijini ni mambo ambayo yanatukatisha tamaa.

Kuhusu maisha ya vijijini, tunaona kuwa, badala ya watu kufanya kazi kwa bidii ili waweze kujitegemea, wanapoteza muda mwingi wakilewa. Ulevi umeshamiri vijijini. Pombe

inayojulikana kama pombe ya moshi ni marufu sana Ukerewe. Ulevi huu unawafanya watu kutowajibika. Daktari wa Bukonyo analewa kiasi cha kutowahudumia wagonjwa. Naye msichana mdogo anasumbuliwa na ng'ombe kwa sababu baba yake ameenda kulewaTunasikitika kuona kuwa ulevi umewafanya baadhi ya watu kuyakwepa majukumu yao.

Maisha vijijini yametawaliwa na uozo. Maadili yamevunjika. Kuna ukatili vijijini. Vijana wanaomtamani Maltilda, mke wa Kamata, wanampiga Kamata vibaya na kumtupa mtoni. Nia yao ilikuwa kumwua Kamata ili wazini na mke wake. Huu ni unyama. Vijijini kuna ukahaba. Tegemea analala na Kabenga kwa malipo. Kabenga analalamika kwa sababu ya Tegemea kuwa na tamaa ya pesa. Anamwambia:

> Una tamaa sana ya pesa.... huku shamba mwanamke hanunuliwi.
> Lakini mimi umenimalizia karibu pesa zote...(uk.79)

Tegemea haoni haya hata kulala na vijana wadogo kama Kalia; bora tu wampe pesa. Naye Nyabuso, anatembea na wanaume mbalimbali. Anajiuza ili apate pesa. Wazazi wake wanatunzwa kwa pesa hizo hizo. Kenyatta (1978:314) anasema kuwa, maadili katika jamii hutegemea mfumo wa uchumi na wa kijamii. Kuvunjika kwa maadili kunaweza kuwa zao la mabadiliko ya kiuchumi katika jamii. Ingawa Nyerere alikuwa ameshaanzisha mfumo wa ujamaa katika jamii ambayo mwandishi anazungumzia, athari za ubepari zilikuwa zingalipo. Ubepari ambao huthamini pesa sana na kusababisha matabaka kwa kuwa ni wachache tu wanaomiliki rasilmali huwafanya wasio na pesa kutaabika. Hii ndiyo sababu wanawake kama Nyabuso wanajiuza ili wapate pesa.

Aidha, kuna uhasama ambao umesababishwa na suala la shamba. Mfumo wa ujamaa uliruhusu mtu kulima mahali popote kwa sababu ardhi ilikuwa mali ya serikali. Familia ya Mafuru inapohamishwa na serikali kwa shamba ambalo awali lilikuwa la Kabenga, uhasama unachipuka. Ni kwa sababu hii ambapo familia ya Kabenga inatafuta mbinu ya kuwafukuza kina Mafuru. Kazimoto anapogundua kuwa Kabenga ndiye aliyekuwa akiwahangahisha, analipiza kisasi kwa kuichoma nyumba ya Kabenga.

Watu vijijini wanaishi kwa hofu kwa sababu kuna wachawi. Familia ya Mafuru inaishi kwa hofu kubwa wakati wanafanyiwa mazingaombwe na familia ya Kabenga. Wanaishi maisha ya kukata tamaa kwa kuwa hawajui wafanye nini dhidi ya watesi wao. Wakati wowote mbwa walipobweka, mama pamoja na watoto walijikunyata kwa woga. Hata Kazimoto alishindwa na la kufanya. Anakiri, 'sijui nifanye jambo gani ili niweze kuwakomesha!' (uk. 3). Watoto wana hofu kiasi kwamba hawataki kuongea juu ya kisa hicho. Kazimoto anaeleza hofu yake. Anasema:

> Hofu kubwa ilinipata kama kwamba simba wa Tsavo walikuwa mbele yangu. Hofu yangu ilikuwa kubwa zaidi.... wala sikufahamu hatari iliyokuwa mbele yangu (uk. 3)

Mwandishi anatumia tashbihi ili kutuwezesha kuhisi namna hofu iliyompata Kazimoto ilikuwa kubwa. Ni kama hofu ya mtu aliyekutanan na simba. Kwa wadhanaishi, hofu kuu au kihoro hutawala maisha ya binadamu.

Kadhalika, kuna ubakaji hata vijijini. Kalia anajifunza tabia ya kulala na wasichana kutoka kwa kakake – Kazimoto. Mwishowe anaanza kuwanajisi wanawake. Matendo yake maovu yanasababisha kifo chake. Anauawa na kutupwa mtoni. Kifo cha Kalia kinaonyesha vile uchaguzi au uamuzi wa mtu unaweza kusababisha madhara. Kwa kuchagua kuwa 'nunda mla watu', Kalia anakutanana na mwisho wake. Vilevile, wazo la wadhanaishi kuwa binadamu hana njia ya kuyakwepa madhara yatokanayo na uchaguzi aufanyao linajitokeza.

Wizi pia unashuhudiwa vijijini. Tegemea anapatikana akiiba viazi shambani mwa Mafuru. Hii ni ishara kuwa kuna umaskini vijijini. Kwa jumla, maisha ya vijijini yamevurugika. Ni maisha duni ambayo hayaridhishi. Vifo vya mara kwa mara, maovu kama vile unajisi, ukahaba, ulevi, wizi na kadhalika unafanya maisha yenyewe yasiwe ya kutamanika. Maovu haya yote ambayo yanaendelea vijijini ni ishara ya kuvunjika kwa maadili na kukosekana kwa utulivu katika jamii. Hizi ni athari za udhanaishi.

Isitoshe, maisha haya yanaonyesha matarajio ambayo hayakufikiwa. Raia walio wengi walitarajia kuwa baada ya uhuru, mazingira ya kiuchumi, kisiasa na hata kijamii yatabadilika

kwa manufaa yao. Miaka michache baada ya uhuru, Rais Nyerere alibadilisha mfumo wa utawala. Badala ya ubepari, alianzisha ujamaa. Hata hivyo, athari za ubepari zilikuwepo miaka mingi baada ya kuanzishwa kwa ujamaa. Ingawa Waafrika ndio wanaojitawala, jamii Tunakatishwa tamaa kuona kuwa serikali ambayo ingeleta usawa baada ya uhuru inaendeleza ubaguzi. Mzee mmoja anamuuliza Kazimoto:

> Sasa uhuru tunapata. Kwa nini serikali haiwezi kutengeneza pesa nyingi sana ili kila mtu awe tajiri? (uk.59)

Kwa upande wa maisha ya mijini, Kezilahabi anaonyesha kuwa maisha hayo nayo yana matatizo yake. Kuna ukosefu wa maadili. Pili ni kahaba ambaye anaishi mjini na ndiye anawaambukiza Kazimoto na Manase ugonjwa wa zinaa. Naye Tegemea kabla ya kuhamia kijijini Ukerewe, alikuwa mtalaleshi huko mjini. Mbali na ukahaba, mijini kuna visa vya unajisi. Moyokonde alimwokoa Vumila kutoka kwa vijana wawili waliokuwa wakimnajisi kwa madai kuwa amechukua pesa zao. Hao vijana pia walikuwa na nia ya kumuua baada ya kumanajisi (uk.190). Kisa hicho basi kinaonyesha ukosefu wa utu. Utu umekosekana mijini kiasi kuwa mtu anauawa kwa kukatakatwa na nyama yake inauziwa wanaochoma mishikaki. Huu ni ukatili iliokithiri. Ubakaji, umalaya wizi na ujahili unaopatikana mijini unaonyesha uvunjifu wa maadili na kukosekana kwa ushwari mijini. Mambo haya yanawafanya wengi wanaoishi mijini kukata tamaa ya kuwa na maisha yenye amani.

Aidha, mijini pia kuna umaskini. Maisha ya Vumilia baada ya kutoka nyumbani (Ukerewe) yanathibitisha hoja hii. Amekonda sana na akabadilika kiasi kuwa Kazimoto hamtambui mara moja. Mashaka yake yanaonekana hata usoni. Tunaelezwa:

> Mwanamke maji ya kunde, mrefu na mwenye uso mviringo ulioonyesha hali ya masikitiko, alitukaribisha ndani... ingawa alikuwa mja mzito mikono yake haikuwa na nyama (uk.182)

Chuku anayoitumia mwandishi inatufanya tupate picha ya Vumilia na tumhurumie. Ni picha ya mtu anayepitia dhiki maishani. Kwa mujibu wa wanaudhanaishi, shabuka ni sehemu ya maisha

ya binadamu. Shida zinazomkabili binadamu huyafanya maisha yake kuwa duni na yasiyokuwa na maana. Mandhari ya nyumba yake Vumilia pia yanaashiria umaskini na uduni wa maisha. Ni kijumba kidogo ambacho kimeezekwa kwa madebe yaliyojaa matunda. Tegemea anakiita kibanda cha kuku. Anauliza:

> Na kwa nini mnaishi katika nyumba kama hii? Sisi kwetu nyumba kama hii ni ya kuku (uk.192)

Vifaa vilivyomo ni vichache tu. Vumilia mwenyewe anakiri kuwa maisha yake ni magumu. Mumewe Moyokonde vilevile amevaa mararu. Haya ni mandhari kinyume na yale yanayopatikana kwa familia ya Manase na Kazimoto ambao pia wanaishi mjini. Hawa wanajiweza kiuchumi. Ni wazi kuwa jamii anayozungumzia mwandishi ina matabaka.

Mwandishi ametamauka kwa kuona kuwa watu wamedunishwa kiasi cha kuishi kama wanyama. Iwapo watu wataishi maisha sawa na kuku, ambao huthaminiwa tu kama chakula, basi maisha yana maana gani? Kulingana na Kingston (1961:192), wadhanaishi wote wanaamini kuwa uhalisia wa binadamu katika ulimwengu huu umedunishwa kabisa. Taswira ambayo inajengeka kutokana na maisha ya Vumilia na mumewe Moyokonde hakika ni ya umaskini unaotamausha. Hawa wanalazimika kuishi katika hali duni ya maisha na hakuna matumaini ya hali yao kubadilika. Vifaa vya kimsingi kama vile nyumba, chakula na nguo havipatikani kwa urahisi. Hakika huu ni uchochole unaokatisha tamaa. Maisha yao yanatufanya tuwe na maswali sawa na ya wanaudhanaishi ambao husaili kuhusu thamani ya maisha na nafasi ya binadamu ulimwenguni.

## 2.2 KUATHIRIWA KWA MWANDISHI NA MAZINGIRA MBALIMBALI

Nadharia ya kisosholojia huwa inatilia mkazo hoja ya kusaili mazingira ambamo kazi ya fasihi ilimoibuka na maisha ya mwandishi. Sababu ni kwamba, mazingira haya na maisha ya mwandishi huathiri mtazamo wake wa maisha. Kezilahabi kama mwandishi wa jamii, ameathirika na mazingira ya kijamii na athari hizi zimejitokeza katika kazi zake.

Mwandishi alishuhudia hali ngumu ya maisha miongoni mwa jamii yake katika nchi ya Tanzania. Hali ya kiuchumi nchini mwake ilikuwa duni na watu wengi walilazimika kuishi maisha yasiyotamanika. Sio matatizo ya kiuchumi tu ambayo yaliikumba nchi hiyo. Matatizo ya kijamii kama vile wizi, ukahaba, mauaji na kadhalika yalikuwepo. Maovu haya mara nyingi huwa matokeo ya hali duni ya kiuchumi. Hivyo, matatizo haya yanakuwa kama duara ambayo inamzunguka binadamu na yanasikitisha.

Matatizo haya yalimfanya Kezilahabi aione nchi yake ikiwa katika hali ya kukatisha tamaa. Huenda mwandishi aliilinganisha hali ya nchi yake na ile hali iliyotawala Ulaya baada ya Vita Vikuu Vya Pili vya Dunia iliyoibusha udhanaishi. Wakati wa vita hivyo, uharibifu mwingi wa mali ulishuhudiwa. Jamii zilivurugika na maadili yakavunjika. Watu wengi pia walipoteza maisha yao. Waliosalia walihisi kuwa maisha hayakuwa na maana kutokana na ugumu wake. Wengine walidai kuwa Mungu hakuwepo kwa maana kama alikuwepo, hangewaruhusu kuteseka jinsi walivyoteseka.

Ni katika misingi hii ambapo wanafalsafa walianza kujiuliza juu ya umuhimu wa maisha ya binadamu, na hivyo udhanaishi ukaibuka. Kama asemavyo Mungah (1999:85), hali hiyo ya mataifa ya Magharibi ambayo ilizua udhanaishi ni tofauti na mazingira ambayo Kezilahabi aliandikia. Hata hivyo, matukio ya kihistoria yaliyokaribiana na hali hiyo yalitukia nchini Tanzania na yakamwathiri mwandishi huyu. Tangu enzi za Ukoloni, nchi hii ilikumbwa na matatizo mbalimbali. Chini ya utawala wa Mjerumani, wenyeji waliishi maisha ya umaskini na unyonge kutokana na kunyimwa haki na kudhulumiwa. Kudhulumiwa huku kuliwafanya wenyeji kuishi katika hali ya utumwa.

Ili kukata minyororo ya utumwa, walianza vita vya ukombozi. Vita hivi vilisababisha vifo vya watu wengi pamoja na uharibifu wa mali. Ingawa uharibifu huu haukuwa sawa na ule ulioshuhudiwa huko Magharibi, uliongezea matatizo yaliyokuwepo nchini Tanzania.

Baada ya kuupata uhuru, wenyeji wengi wa nchi za Kiafrika, wakiwemo Watanzania walitarajia kuwa maisha yao yangekuwa bora chini ya utawala mpya wa Waafrika wenzao. Walikuwa na

matumaini makubwa kwamba wangepiga hatua kubwa kimaendeleo, wamalize umaskini na pia walitazamia kukomesha udhalimu.

Kinyume na matarajio haya, hali baada ya uhuru ilibakia ile ile kwa mwananchi wa kawaida. Hoja hii inatiliwa uzito na Fage na Oliver (1984:385) wanaposema yafuatayo kuhusu nchi ya Tanzania:

> Uhuru wa bendera hata hivyo, haukubadilisha ruwaza ya maendeleo kwa muda, asasi mbalimbali zilizorithiwa kutoka kwa mkoloni ziliendelea, vilevile hali ya umaskini. Ugawaji wa mali ghafi ulikuwa hauzingatii usawa.

Waliofaidika tu ni wale waliokuwa na vyeo serikalini. Udhalimu uliendelezwa na wenye vyeo. Manase kama Mkuu wa Wilaya hawahudumii wananchi kwa njia inayostahili. Anamfukuza mzee mmoja kutoka ofisini mwake kwa sababu ya kuingia mle akiwa na fimbo (uk. 7).

Maendeleo hayakupatikana hata baada ya uhuru. Huduma za kimsingi kama vile maji safi zilibakia ndoto. Wanakijiji wanaogea kisimani kisha wanachota maji mumo humo. Huduma za afya katika jamii hii pia hazikuimarika. Baadhi ya watoao huduma hizo kama vile daktari wa Bukonyo, si wa kutegemewa. Wanalewa hata wakati wa kazi. Vilevile kuna uhaba wa madaktari. Daktari aliyetibu ugonjwa wa Manase anapofariki, panakosekana mwingine wa kuwatibu wengine wenye ugonjwa kama huo. Kazimoto anamuuliza Manase,

> "Ninaweza kumwona hata mimi?"
> "Bahati mbaya sana, Kazimoto, huyo daktari alikufa juma lililopita na watu waliopelekwa kusafisha nyumba yake ili mwingine aingie walichoma vidonge vyote hivyo bila kufahamu. Sasa hapatikani tena daktari yeyote." (uk. 213)

Barabara hazikutengenezwa. Wasafiri wanalalamika kuwa wanaumwa na mgongo kwa sababu ya barabara mbovu (uk.16). Umaskini uliendelea. Mzee mmoja anamuuliza Kazimoto,

> Zamani Mkoloni alikuwa akitengeneza pesa kidogo kwa sababu alikuwa hataki tuendelee na alikuwa akituonea...Sasa uhuru tumepata. Kwa nini serikali haiwezi kutengeneza pesa nyingi sana kila mtu awe tajiri? (uk.58)

Nukuu hii inaonyesha kuwa hali kabla ya uhuru haikuwa tofauti na hali baada ya uhuru. Ni hali inayotamausha kwa mwananchi wa kawaida. Baada ya uhuru, Rais Nyerere aliamua kuanzisha siasa za Ujamaa. Mnamo mwaka wa 1967, Azimio la Arusha lilibuniwa. Kulingana na Mungah (1999:88), siasa za ujamaa zililenga katika kuleta usawa wa binadamu na kuondoa matabaka katika jamii. Hata hivyo, ni wazi kuwa malengo haya hayakufanikiwa na jamii iliendelea kuwa na matabaka ya wenye mali kama vile Manase na Kazimoto na maskini walioishi kwenye ufukara uliokithiri. Hawa ni kama vile Vumilia na Moyokonde.

Kuwepo kwa shida ainati kuanzia enzi za Mkoloni pamoja na kutofaulu kwa nchi yake hata baada ya uhuru kulimfanya Kezilahabi achukue mwelekeo wa kiudhanaishi. Kezilahabi aliona kuwa jamii yake haijapiga hatua kubwa kimasomo. Ni wachache tu ambao walikuwa wamesoma. Masomo na hasa masomo kwa wasichana hayakutiliwa maanani sana. Wasichana wengi waliozwa badala ya kuendelea na masomo. Wazazi wa Rukia walinuia kumwachisha shule ili aolewe lakini Kazimoto akamtetea (uk.23) Hata mfumo wa elimu ambao ulikuwa unafuatwa haukuwa na manufaa kwa jamii. Wale walioupitia mfumo huo waliishia kukengeuka na kupotosha jamii. Mfano ni Kazimoto na Manase. Hali ya nchi yake hata baada ya uhuru haikuelekea kuwa bora zaidi. Ilikatisha tamaa. Alishuhudia matatizo mengi yaliyoendelea kuikumba nchi yake na wenyeji wake. Haya yalimfanya aone kuwa binadamu ametupwa katika ulimwengu uliojaa dhiki zisizoepukika. Kwa mujibu wa Mungah (1999:91) shida chungu nzima ambazo Kezilahabi aliendelea kushuhudia zilimpelekea kuipaka dunia rangi ya fujo, vurugu na vurumai tupu.

Aidha jamii ya mwandishi ilikumbwa na matatizo ya kimaadili. Maovu kama vile unajisi, usherati, wizi, ulevi, uhasama na kulipiza kisasi ni mambo ambayo yalijitokeza katika jamii ya mwandishi. Yumkini shida ambazo mwandishi alishuhudia miongoni mwa jamii yake zilimwathiri na zikamfanya auone ulimwengu kama pahala pasipofaa maisha ya mwanadamu.



UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION
JOMO KENYATTA MEMORIAL
LIBRARY

Haya ni maoni ambayo yanaenda sambamba na maoni ya wadhanaishi kama vile Albert Camus na Samuel Beckett. Hawa walimwona binadamu kama kiumbe aliyewekwa katika ulimwengu duni wenye maswala mengi yanayomtatiza.

Kezilahabi kama mwandishi aliathiriwa na kazi za waandishi waliokuwa na mtazamo wa kidhanaishi. Sawa na asemavyo mungah (1999:84), mtazamo wake wa kidhanaishi na hasa kuhusiana na swala la Mungu, unaweza kuwa uliathiriwa na maisha yake ya shuleni. Kwa mujibu wa Mulokozi (1983:1), Kezilahabi alisomea katika Seminari ya Kikatoliki ya Nyegezi. Hata hivyo, hakumaliza masomo hayo. Alifukuzwa baada ya walimu wake kusema kuwa hakuwa na wito wa kutosha wa kuwa padre. Huenda hii ndiyo sababu mwandishi huyu anaipuuza dini na kutia shaka kuwepo kwa Mungu. Kupitia kwa mhusika Kazimoto, Kezilahabi anasema kuwa huenda Mungu hayupo (uk.59). Anaendelea kusema kuwa woga unaoletwa na mambo yote yanayomzunguka binadamu ndiyo huzua dhana ya Mungu.

Wadhanaishi wengine ambao wamepuuza dini na ambao bila shaka wamemwathiri Kezilahabi ni pamoja na Jean-Paul Sartre ambaye alidai kuwa 'Mungu amekufa' na Friedrich Nietzche aliyedai kuwa kanisa ni kaburi la Mungu.

Wamitila 1997:16 amesema kuwa katika mazungumzo kati yake na Kezilahabi, Kezilahabi alikiri kuathiriwa pakubwa na waandishi Martin Heidegger na Friedrich Neitzche ambao ni wadhanaishi. Baschiera (2003) vilevile anasema kuwa Kezilahabi anatazamwa kama mdhanaishi ambaye ameathiriwa na falsafa ya Heidegger na Nietzche katika kuandika juu ya maisha ya binadamu kwa jumla. Heidegger anamwona binadamu kama kiumbe asiyekuwa na uwezo juu ya matukio ya maisha yake. Athari za mdhanaishi Heidegger zinaonekana katika kazi za Kezilahabi. Kupitia kwa mhusika Kazimoto, mwandishi anaonyesha udhaifu wa mwanadamu dhidi ya matukio maishani. Analinganisha maisha na maji ya mto yateremkayo baharini bila uwezo wowote wa kurudi nyuma (uk.102). Anatumia mfano huu kuonyesha kuwa maisha ya mwanadamu yanaendelezwa na nguvu ambazo yeye binafsi hawezi kuzidhibiti. Hivyo, matukio maishani mwake yanakuwa kama ajali tu.

Jamii ndiyo impayo msanii msukumo wa kuandika. Huenda mwandishi huyu alisukumwa na matatizo aliyoyaona katika jamii yake akayalinganisha na matatizo yaliyojadiliwa na waandishi wengine wa kidhanaishi na akaona kuwa maisha ni dhiki tupu. Katika kazi yake hii, kama kazi nyingine zake, msomaji anabaki bila matumaini yoyote. Kama anavyosema Mungah (1999:98), watu wengi hawapendezwi na jinsi Kezilahabi anavyojadili na kuyagubika giza masuala ya maisha, kifo, ukweli, furaha, Mungu na uasi wa dini.Aidha, wengi wanaikashifu falsafa yake inayomsawiri binadamu kama kiumbe aliyeumbiwa mateso.

## 2.3 Hitimisho

Katika sura hii, tumechunguza athari za udhanaishi katika *Kichwamaji.* Tumeona kuwa sawa na udhanaishi ambao hujishughulisha na swala la maisha ya binadamu na nafasi yake duniani, swala la maana ya maisha ya binadamu limechukua nafasi kubwa katika riwaya hii. Mwandishi ameonyesha wazi kuwa maisha yamejaa usumbufu ambao unamvunja moyo mwanadamu. Aidha, shida nyingi kama vile umaskini, magonjwa, kifo na kadhalika ambazo zinakumba binadamu huyafanya maisha kukosa thamani.

Sawa na wadhanaishi ambao humulika mwanadamu katika safari yake ya maisha, Kezilahabi pia ameonyesha safari ya maisha kupitia kwa wahusika wake. Tunayaona maisha ya Kazimoto ambayo yanakuwa magumu kiasi kwamba hayastahimiliki tena. Kazimoto anajiua kwa kuwa haoni maana ya kuendelea na maisha. Mbali na maisha kukosa maana kwa sababu ya ugumu wake, tumeona kuwa hakuna matumaini ya hali nzuri. Kazimoto anatamauka na kujiua kwa kufahamu kuwa ugonjwa wake haungetibika. Inavunja moyo kufahamu kuwa hata baada ya kifo cha Kazimoto, shida inayomfanya ajiue itaendelea. Kupitia kwa mtoto wa Manase, kizazi chenye vichwa vikubwa kitaendelea. Hii ni hali inayokatisha tamaa. Riwaya ya *Kichwamaji* inatamausha. Haitoi mwanga wowote wa hali kubadilika na kuwa bora zaidi. Aidha, katika sura hii tumeangalia mazingira ambayo yamemwathiri mwandishi na kumfanya achukue mwelekeo wa kidhanaishi.

# SURA YA TATU

## UDHANAISHI KATIKA *NGUVU YA SALA*

### 3.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tumeshughulikia udhanaishi katika riwaya ya *Nguvu ya Sala*. Tumefanya hivyo kwa kuyamulika masuala mbalimbali ambayo kazi hii imeyaibusha. Aidha, tumejaribu kuoanisha athari za udhanaishi ambazo zimejitokeza na mazingira ya kijamii anamotoka mwandishi.

### 3.1 MAUDHUI

#### 3.1.1 Malezi

Malezi ni sehemu muhimu ya maisha ya mwanadamu. Kila mzazi ana jukumu la kumlea mtoto wake kwa njia itakayomwezesha kukubalika katika jamii, na aweze kukabiliana na maisha yake ya baadaye.

Richard pamoja na mkewe Mary, wanawalea watoto wao wanne (Wasichana) kwa njia inayokatisha tamaa. Ingawa malezi ya wazazi hawa yanazingatia mafundisho ya Biblia, ni malezi ambayo hayajakamilika. Richard anajizatiti kwa matumaini kuwa familia yake itakuwa kielelezo cha kuigwa na wanajamii. Kwake, hili litawezekana tu kupitia kwa nguvu ya sala ambayo inakuwa mhimili wa familia hii.

Hivyo, Richard anaegemea upande mmoja tu na kuyapuuza mambo mengine ambayo ni muhimu katika malezi ya watoto wake. Naye Mary, mkewe Richard, amekuwa kasuku wa kusisitiza tu yale mumewe amesema. Kwa sababu hii watoto wa familia hii wanakosa wa kuwaongoza katika nyanja zote za maisha. Malezi wanayopata mabinti wa Richard yamewanyima uhuru wa kukua kama watoto wengine. Hawatakiwi kucheza na watoto wa majirani ambao si Wakristo. Susan

anapokiuka amri ya babake na kucheza na watoto wa jirani, anapokea kipigo ambacho athari zake zinaonekana hata siku iliyofuata. Mwalimu wao Susan anaelekea kushangazwa na sababu anayoitoa Susan ya kupigwa. Susan anapomweleza kuwa alipigwa na babake anamuuliza:

> "Kwa sababu gani?"
> "Nilicheza na watoto wa jirani"
> "Hilo tu?"
> "Mm….. amesema kuwa hatuna ruhusa ya kucheza nao"
> (uk 4) (msisitizo wetu)

Vilevile, hawapaswi kutangamana na wenzao bila ruhusa. Baada ya kumaliza mtihani wa darasa la nane, Susan na wenzake wanaamua kwenda matembezi. Anaporudi wakati wa magharibi, anapigwa vikali hadi anajikojolea. Licha ya kukatazwa kufanya mambo fulani, watoto hawa hawakuelezwa sababu ya kutoshiriki katika mambo walioyatenda wenzao. Susan anaeleza:

> Nilishangaa kwa nini baba hakutaka kuniruhusu nijiunge na wenzangu. Labda alikulia katika mazingira kama hayo…. (uk. 24)

Aidha, hawaruhusiwi kucheka kwa sauti ya juu, kwani kulingana na baba yao, hiyo ni tabia mbaya hasa kwa mtoto wa kike. Kucheka hivyo kuliandamana na adhabu kama alivyotambua Susan aliposikika na babake akicheka (uk 33).

Susan alishaanza kuuona udhaifu wa malezi ya wazazi wake. Anapomwangalia dadake Roselyn, anasema:

> Bila shaka angetamani kwenda matembezi au kwenda kucheza mwajificho na rafiki zake… Haikosi angetamani kuandamana na vijana wenzake huko maporini kwenda kukata kuni na kucheza mchezo wa baba na mama au kuiga sauti na mili ya ndege mbambali. *Lakini*

*asingeweza kufanya haya kwa sababu hapakuwa na ruhusa ya kutoka nyumbani. Baba alikuwa mchelevu wa kutoa idhini hiyo*… uk 107

Watoto wake Ngunze hawakuwa na uhuru wa kuhusiana na wavulana. Susan alishauriwa na mamake kuwa ilimlazimu atahadhari na wavulana. Inakuwa balaa anaposindikizwa na James, binamuye Bethseba. Baada ya kumaliza masomo ya kidato cha nne, Susan anasindikizwa na Cedric lakini hangetaka huyu amfikishe nyumbani kabisa. Anasema:

> Sikutaka aonekane na baba. Nilichelea maneno ya baba; sikutaka kuaibishwa mbele ya msomi huyu ambaye nilimwona muungwana ingawa nina hakika baba angemwona vingine kabisa. (uk 128).

Ni wazi kuwa Richard angemkemea binti yake kwa kumwona tu na mvulana. Yaelekea hakujali hisia za binti yake kamwe. Anawachunga mithili ya mahabusu. Wanapokwenda mahali, lazima waandamane na kitinda mimba, Redemta. Huyu ndiye angetoa ripoti yoyote kuhusiana na mienendo ya dada zake. Roselyn anapomwandikia Susan barua anamwambia kuwa huko shuleni 'hatuchungwichungwi kama vifaranga walindwavyo dhidi ya nguchiro, kanu na kipungu' (uk 185).

Hii ni ishara kuwa hata Roselyn anayakejeli malezi ya wazazi wake, yanayowanyima uhuru. Udhanaishi unamhimiza binadamu ajitegemee na kuupigania uhuru wake kwa vyovyote vile. Mabinti wa Richard, ambao wamenyimwa uhuru wanaamua kujitafutia na kuupigania uhuru wao. Roselyn anasema kuwa mtu akinyimwa uhuru hujitwalia (uk. 187).
Naye Susan anaongezea kwa kusema:

> Binadamu hutaka uhuru na yeyote ambaye anakulia katika mazingira ya mfungwa uchochewa wazi na mazingira hayo hayo kuasi *Penye uhuru hapawi na uasi* (uk 197) (msisitizo wetu)

Kwa sababu ya kunyimwa uhuru, Roselyn anaamua kuasi. Matokeo yake ni mimba akiwa kidato cha pili. Hili linampelekea kufukuzwa nyumbani. Hata hivyo, Susan ambaye ameamua 'kuasi' kwa kutofuata kila kitu ili kupendeza babake anamtetea mnuna wake na anarudi nyumbani.

Haya ni mawazo yanayooana na ya wadhanishi. Udhanaishi hukubali uhuru wa binadamu na kukataa dhana zenye misingi ya kijamii inayodunisha kuwepo kwa uhuru wa binadamu. Huwasilisha maasi dhidi ya mawazo na asasi ambazo huzuia uhuru wa binadamu na kupinga uwajibikaji. (Encylopaedia Americana 1977:762) Tasfiri yetu.

Hakika haya ndiyo Roselyn na Susan wanasema. Kila binadamu anapaswa kuwa huru kujichagulia. Katika malezi yake, Richard amefanikiwa tu kuijaza familia yake hofu. Hofu kuu au kihoro ni sifa mojawapo ya udhanaishi. Hofu kwa watoto wa Richard inatokana na adhabu ya mara kwa mara. Maisha ya jamii yake yametawaliwa na fadhaa. Vitendo vya kawaida vya watoto kama vile kucheza na kucheka vinawafanya watoto wa Richard waadhibiwe. Kwa mujibu wa Richard vitendo hivi ni makosa. Inaelekea kuwa 'kosa' la mtoto mmoja linazua adhabu kwa wote. Susan anapocheza na watoto wa jirani, anapigwa sana kisha anamrishwa anyamaze. Wadogo zake ambao walikuwa wakilia pia walinyamaza. Siku hiyo, watoto wote walilala njaa. Kama anavyoarifu Susan:

> Siku hiyo hatukula. Hiyo ilikuwa adhabu yangu ya kucheza na watoto wa jirani.... Usiku sikulala; njaa ilinisumbua sana. Ilinibidi kuvumilia. Wadogo zangu walishindwa kuvumilia; walikesha kulia (uk 3).

Kwa watoto hawa baba ni jina lililowatia hofu sana. Susan anapoambiwa kuwa baba amemuulizia, hofu inamtambaa mwili mzima. Wadogo wake Susan hawana ujasiri wa kumwangalia anapoteteshwa na babake. Wana hofu kuwa kitendo hicho cha kumwangalia kinaweza zusha balaa. Hawana hakika na matendo yao. Roselyn anachapwa kwa sababu ya kuvaa ushanga. Hawatakiwi kusikiliza au kucheza nyimbo sisizo za kumtukuza Mungu. Hii ndiyo sababu Roselyn anakuwa mwangalifu sana anapocheza. Tunaambiwa:

> Alichelea kukutwa seli na babake; ingekuwa kiama kama angetekwa bakunja akiuchezesha mwili wake (uk. 110).

Tunastaajabu kuona kuwa Susan anamwogopa babake kuliko mwalimu. (uk. 4) Hofu yenyewe inatokana na ukali wa baba. Susan alishaonywa kuhusiana na tabia ya kuuliza uliza. Anaeleza:

> Nilishawishika kumwuliza baba. Lakini nilighairi, lazima - angechukia, tena sana. Hivi majuzi alinionya dhidi ya kuwa na tabia ya udadisi. Alisisitiza kuwa tabia hiyo ingenipelekea kuwa na umbea (uk. 10).

Hivyo, Susan anabaki na maswali ambavyo yanamsumbua akilini. Mama hampi majibu ya kuridhisha na hata anamnyamazisha wakati mwingine (uk. 10). Malezi ya Richard na Mary yana upungufu kwa sababu yanawapa watoto wao maongozi ya kiroho tu. Hatuwaoni wakiwaelekeza watoto wao katika njia ambayo itawasaidia kukabiliana na matatizo ya ulimwengu. Wanachosisitiza wazazi hawa ni nguvu ya sala kana kwamba matatizo yote yatasuluhishwa kwa maombi tu. Wanakwepa kuwatayarisha watoto kwa uhalisia wa maisha na jambo hili linawatatiza mabinti hawa si haba. Susan anapokaribia kuingia shule ya upili, anapewa mawaidha na wazazi wake. Anashauriwa ajitunze ili asimwaibishe babake. Vilevile alihimizwa asiisahau nguvu ya sala pamoja na kuwa alikuwa mtoto wa nyumba ya Kikristo.

Mamake hakujishughulisha na kumweleza Susan kuwa kama msichana, angepitia mabadiliko ya aina fulani maishani. Hii ndio sababu Susan anahangahika sana anapopata hedhi kwa mara ya kwanza. Hata anafikiria kuomba kutamtatulia tatizo hilo kama alivyoshauriwa na wazazi. Rafiki yake Bethsheba ndiye anamfahamisha kuhusu hali yake na namna ya kujitunza. Mary Kasiva, mamake Susan amekosa kutekeleza wajibu wake kama mzazi na Susan analalamika:

> Mawazo mengi yalinitorora akili. Sikumbuki siku hata moja ambapo mama alinielezea hali kama iliyonikuta leo na kunifanya nikose vipindi vya alasiri (uk. 61).

Huu ni udhaifu kwa upande wake Mary. Udhaifu huu unatambuliwa na Susan anaposhikwa mkono na mwalimu mkosa mbeko: Octavian Birundu. Anashtuka sana. Anaona kuwa kuna mengi kuhusu mabadiliko ya kimaumbile ambayo mama hakumwelezea (uk. 80). Siku hiyo alifikiria sana na akaona fika kuwa palikuwepo na upungufu fulani katika maisha yake. Anawalaumu wazazi wake kimoyomoyo kwa kukazania jambo moja tu: nguvu ya maombi. Anasema:

> Nilianza kuhisi kuwa mwito wa baba wa nguvu ya sala
> ulikuwa na mpwayo na mterereko fulani. (uk. 80)

Baadaye, Susan anawaeleza wazi kuwa hakuwa na imani na malezi ambayo waliwapatia. Baada ya Roselyn kufukuzwa nyumbani sababu ya uja uzito, Susan anamtetea dadake. Anawalaumu wazazi kwa kutomwongoza vyema. Anasema:

> Kama kuna makosa yoyote, yamo katika malezi mliyotupa. Mmekazania tuyafuate mafundisho ya Biblia bila ya kutuelekeza katika maisha halisi ya ulimwengu huu. (uk. 196)

Susan anawalaumu wazazi wake kwa msiba unaomsibu mnuna wake. Kama angekuwa ameelekezwa vyema, yasingemfika yaliyomfika. Hivyo malezi haya hayajafanikiwa. Mimba ya Roselyn ni ithibati. Kupitia kwa malezi haya tunaona udhaifu wa binadamu. Richard anajaribu kutimiza lengo lake la kuwa na familia kielelezo cha kuigwa, lakini hili haliwi. Hii ni athari ya udhanaishi. Kama asemavyo Warnock Mary, juhudi za binadamu huwa bure kwani mwishoni mtu hana budi kukikosa kile ambacho amekidhamiria.

Yumkini Wamitila alikerwa na mambo ambayo alishuhudia katika jamii yake. Kuna baadhi ya wazazi ambao hawapatii watoto malezi yaliyokamilika. Wengine hudhani kuwanunulia watoto nguo na vyakula tu kumetosha. Hili hutokea mara nyingi katika familia ambazo wazazi wote wawili wanafanya kazi. Jukumu kubwa la malezi linaachiwa wafanyi kazi wa nyumbani. Anawashauri wazazi wawe na muda na watoto wao, wawajali kwa kila njia na wawaelekeze katika nyanja zote za maisha. Endapo

hawatafanya hivyo, basi maisha ya watoto wao yatatatizika; kwani asiyefunzwa na mama hufunzwa na ulimwengu. Mara nyingi ulimwengu hufunza kwa kuadhibu. Kwa ujumla malezi ambayo yamesawiriwa katika riwaya hii yanatamausha.

### 3.1.2 Uozo wa Jamii

Jamii ambayo imesawiriwa na mwandishi wa *Nguvu ya Sala* imepotoka kimaadili. Kuzorota kwa maadili ni mojawapo ya athari za udhanaishi. Maovu ambayo tunashuhudia katika jamii husika ni mengi. Katika shule ya upili ya Miwani, ambapo Susan ni mwanafunzi, tunakutana na mwalimu mkosa mbeko: Octavian Birundu. Huyu alikuwa na tabia ya kuwatongoza wasichana na kuwaalika kwake, ingawa sheria ya shule iliwakataza wanafunzi kuenda karibu na nyumba za walimu. Anapowapeleka wanafunzi kuigiza, anamtongoza Susan. Anamwita gizani kisha anamshika mkono. Susan anapomkatalia hila zake, anazidi kumshawishi. Anamwambia:

"Mm.... Suzie hu mtoto tena. Ni nini unachoogopa? (uk 79)

Susan anapomkataa kabisa, anatumia wanafunzi wengine ili ampate. Anawapa pesa ili waendelee kumshawishi. Rose Mafali anapewa mia mbili pamoja na karatasi ya mtihani ambao haukuwa umefanywa kusudi tu amshawishi Susan kumpenda Birundu (uk. 93). Huu ni uozo wa hali ya juu. Mwalimu huyu anaendeleza vituko vyake na mwishoni anapigwa kalamu kwa sababu ya kumtia mwanafunzi mimba. Hii ni tabia mbaya sana ambayo Birundu alikuwa ameizoea. Susan amesema kuwa hastaajabishwi na kufutwa kazi kwa Birundu kwani, "nzi kufia kidondani si bina" (uk 139).

Naye sista Emily vilevile ni mtovu wa maadili. Huyu sista, ambaye ni mhudumu wa zahanati ya shule anawasaidia wasichana kuavya mimba. Hivyo, alipendwa sana na wasichana wakubwa kama vile Fortunata. Kuna wakati ambapo Fortunata anaugua maradhi ya tumbo yanayomfanya atapike kila asubuhi. Tunaambiwa:

> Maradhi ya Fortunata yalitibiwa na Sista Emily
> Haikosi alikuwa an uzoefu mkubwa wa kazi yake (uk 64)

Sista Emily mwenyewe anakiri kuwa alijihusisha na ngono akiwa bado mdogo. Huu ni utovu wa maadili. Huyu, kama Mwalimu Birundu, anafutwa kazi baada ya kumsaidia msichana wa kidato cha pili kuavya mamba. Ni kinaya kuwa anaitwa Sista. Masista huwa watu waliojitolea katika kudumisha maadili, kinyume na Sista Emily ambaye amepotoka na anawahimiza wasichana kukiuka maadili kwani walifahamu kuwa wana msaidizi wanapoharibikiwa na mambo.

Karibu na chuo kikuu, kunapatikana kijusi ambacho kimetupwa katika pipa la takataka. Hili linamshangaza sana Susan, lakini mwenzake June anamfahamisha kuwa kuna vingine vinne (vijusi) ambavyo vilipatikana katika hoteli moja. Inaelekea kuwa haya ni mambo ya kawaida kulingana na usemi wa June. Alexina anapoeleza kuwa kijusi mtoto kimepatikana, June anasema:

> Mm… Hilo tu nilidhani ni jambo kubwa; *hayo tumeshayazoea katika jiji hili.* Yazuke mengine makubwa (uk. 159).

Ama kweli ni jamii iliyooza na kuozeana ikiwa kuua watoto (vijusi) ni jambo la kawaida.
Aidha, uzinzi unabainika katika jamii ambayo mwandishi ameisawiri. Huko Kibera Laini Saba, Richard anasikia jirani yake akijadiliana na mwanamume. Mjadala huo unaendelezwa hivi:

> Sasa unasemaje" Sauti ya kiume iliuliza.
> "Hamsini itatosha. Ile sauti ya kike ilijibu
> "Mm… La! Hizo ni fedha nyingi mno,"
> Nyingi zipi hizo?.......Yule mwanamke alisema.
> "Nitatoa thelathini"
> "Kama ni thelathini itakubidi utumie mpira
> basi". Alisema yule mwanamke (uk 88).

Haya si mapya kwa Richard kwani yalikuwa yakitukia huko mtaa wa Swahili Machakos, alipokuwa akiishi akiwa mwanafunzi. Uozo unaendelea kuonekana kupitia kwa mahusiano kati ya mwajiri na mwajiriwa. Mary anapoajiriwa na Deogratias, wanaanzisha uhusiano wa kimapenzi ingawa Deogratias ana bibi. Mary anapopata mimba, inatolewa na daktari mmoja huko mjini. Mary anapojaribu kuuvunja ule uhusiano, anatishwa. Mambo yanamwendea kombo wanapofumaniwa na mkewe Deogratias. Anafukuzwa kazini akiwa na mimba nyingine.

Ukabila ni uovu ambao unapaswa kukemewa katika jamii. Richard anautambua ukweli huu baada ya kuajiriwa katika kampuni ya Pombe Breweries. Baada ya miezi sita, mwenyekiti mpya anateuliwa. Huyu analeta sera mpya zilizofanya wengi, hasa wasiokuwa wa kabila lake kuachizwa kazi. Richard hakunusurika. Mwandishi anaubeza ukabila kwa kutumia kinaya. Anasema:

> Labda mtangamano wa jamaa wa kabila moja ulizua
> mtazamo mmoja wa kikazi ambao ungeizidisha tija ya
> kampuni nayo jamhuri ingefaidi kutokana na tija hiyo (uk. 147)

Dondoo hili linaonyesha vile mwandishi alivyokerwa na ukabila. Anawadhihaki wanaoundeleza.

Aidha kuna ufisadi ambao unaendelezwa na viongozi. Kange'the (mkurungenzi mkuu wa benki) anahusika na kashfa ya wizi wa benki lakini anateuliwa kama mwenyekiti wa Pombe Breweries na rais wa jamhuri. Huu ni ufisadi uliozidi. Inavunja moyo kuona kuwa taifa ambalo liko huru linaendeleza ukabila na ufisadi. Vita vya uhuru vilidhamiria kumaliza maovu kama haya.

Mtaa wa Kambi umejaa maovu ya kila aina. Kuna uvutaji bangi, ukahaba, uuzaji wa pombe haramu, wizi, biashara ya vipuli vilivyoibiwa na kadhalika (uk. 147). Ukatili unadhihirika pale ambapo kijana mmoja anaiba pochi ya mwanamke. Ingawa kibogosho hicho hakikuwa na vitu vya maana, kijana huyu anapigwa kipopo na kuumizwa vibaya. Mwishowe fundi mmoja anamuua kwa kukibofya kichwa chake kwa jundo. Unyama ulioje?

Maovu haya yamewaathiri walio wengi katika jamii. Kama anavyosema Rose, ni wachache tu ambao ni waadilifu. Anamwambia Susan:

> Suzie, wanaozifuata sheria hizo au wanaoongozwa na maadili katika nchi hii ni wachache kama wapo (uk. 97)

Wingi wa maovu katika jamii ni jambo la kutamausha. Lakini wa kulaumiwa ni nani? Mfumo duni wa uchumi pamoja na utawala mbaya ndio unaochangia katika maovu haya. Kama asemavyo Susan:

> Watu hawakuyatenda waliyoyatenda kwa mapenzi yao, bali yalikuwa matokeo ya wakati na mfumo wa kijami na kiuchumi uliokuwapo (uk. 184)

Yaelekea mwandishi alikerwa sana na mambo aliyoshuhudia katika jamii yake. Hali ngumu ya kiuchumi kwa walio wengi, utawala unaokandamiza na kukuza ufisadi, kukosa kuwajibika kwa watumishi wa serikali kama vile waalimu na kadhalika. Hakika haya yote hayana budi kumfanya mtu akate tamaa. Katika jamii ambayo inapitia hali ngumu, maadili hayana budi kuvunjwa. Maisha huonekana kutokuwa na maana. Hizi ni athari za udhanaishi.

Udhanaishi uliibuka katika mazingira kama haya. Baada ya vita vikuu vya Dunia, maisha yalionekana kutokuwa na maana kwa sababu ya ugumu wake na kuvunjika kwa maadili ya jamii.

### 3.1.3 Dhana ya Maisha

Kimsingi, falsafa ya udhanaishi hushughulikia swala la maisha. Hujaribu kuonyesha uduni wa maisha ya binadamu katika ulimwengu dhalimu, ambapo hujaribu kutekeleza malengo yake bila mafanikio. Kwa vile binadamu ni kiumbe dhaifu anashindwa kuyadhibiti matukio ya maisha yake. Maisha yanakosa maana kwa vile juhudi zozote za binadamu hazifanikiwi. Ni kama kwamba mustakabali wake umeghubikwa.

Haya ndiyo Wamitila anatonyesha kupitia kwa maisha ya Richard. Ngunze. Ni kupitia kwa mhusika huyu ambapo tunaona vile mwanadamu anashindwa kuyatekeleza malengo yake.

Akiwa katika shule ya upili, Richard alitamani sana kusoma hadi chuo kikuu, ili apate kazi nzuri. Alitamani maisha ya starehe ambapo angekuwa na gari na wasichana warembo. Alisoma kwa bidii ili malengo yake yatimie. Hata hivyo, haya yote hayakuwa.

Matokeo yake ya mtihani yaliathiriwa na mambo ambayo hangeweza kuyazuia. Richard akiwa katika kidato cha nne, anaanza kusumbuliwa na ugonjwa ambao hauponi. Baada ya kuanza mtihani wake wa kidato cha nne, anapokea habari kuhusu kifo cha babake. Ingawa Richard alikuwa na nia ya kurudia mwaka mwingine kusudi aendelee na masomo yake, hakufanikiwa kwa sababu baada ya babake kufariki kulizuka mfarakano katika familia kuhusiana na urithi. Hivyo ndoto yake ya kuendelea na masomo ikakomea hapo.

Baadaye, anaelekea jijini Nairobi ambapo anatarajia kupata kazi. Hakupata kazi ya maana isipokuwa vibarua ambavyo havikudumu kwa muda mrefu. Richard alitarajia kumwoa msichana bikira, lakini anaishia kumwoa mmoja ambaye alikuwa anaibeba mimba ya mtu mwingine. Alitamani sana kifungua mimba mvulana, aliyemranda. Kinyume chake, anapata binti mwenye macho makubwa. Anaudhika sana na tunaambiwa kuwa "alishindwa kumsamehe mke wake" (uk 183).

Isitoshe, Ngunze alikuwa na matumaini makubwa kuwa familia yake ingekuwa kielelezo cha jamaa ifaayo. Alikazana sana kuilea katika misingi ya Kikristo. Hata hivyo, tunasikitika kufahamu kuwa matumaini ya Ngunze yalififia. Binti yake Roselyn anapata mimba akiwa katika kidato cha pili. Mambo haya yote yanatuelekeza katika kutambua unyonge wa mwanadamu maishani kwani juhudi zake zote, huambulia patupu. Hizi ni athari za udhanaishi. Kupitia tajriba za Richard Ngunze mwandishi anatueleza mawazo yake kuhusiana na maisha.

Anatuonyesha uduni wa maisha kupitia mazingira mbalimbali ambamo Richard anajikuta. Akiwa mwanafunzi, Richard anaishi katika mtaa wa Swahili. Hali ya maisha katika mtaa huu si ya kutamanika. Inatamausha. Ni maisha yaliyosheheni dhiki. Kuna watu wengi ambao wanaishi kwenye vibanda vibovu. Kuhusu mtaa wa Swahili tunaambiwa:

> Huu ulikuwa mtaa uliofurika vibanda vya kila aina; vibanda vidogo na mabanda makubwa yaliyojiinamia mbavu za mbwa (uk. 25)

Mwandishi ametumia msemo-mbavu za mbwa kueleza hali dhaifu ya vibanda hivyo. Vibanda vyenyewe vimeezekwa kwa madebe yaliyoliwa na kutu na havina umeme kwa sababu wenyeji wameshindwa kulipa bili. Isitoshe watoto wanaopatikana katika mtaa huu hawana mavazi. Wanachezea maji chafu wakiwa uchi. Hii ni hali ya kusikitisha na inaonyehsa kuwa hali ya kiuchumi ya wanaoishi pale ni duni. Hali si tofauti , katika mtaa wa Kibera Laini Saba. Richard anapoenda jijini Nairobi kwa mara ya kwanza anaishi Kibera Laini Saba. Sawa na mtaa wa Swahili huko Machakos, mtaa wa Kibera una msongamano wa watu wanaoishi kwenye mabanda mabovu. Tunaelezwa:

> Nyumba za mtaa huu zina wasifu wa aina moja; zote nyumba za mabanda ambayo yamejiinamia mbavu za mbwa. Mabanda ya kifusi cha udongo ambao hupukutika kila uchao yaliyoezekwa kwa madebe yaliyochakaa na kuchukua rangi ya kutu. Mabanda yamesongamana kabisa.... (uk 85).

Dondoo hili linasawiri picha ya mahali ambapo hapastahili kama makazi ya binadamu. Uduni wa maisha katika mtaa wa Kibera unashadidiwa na mazingira ambamo mtaa huu unapatikana. Tunaambiwa:

> Mtaa huu umejengwa katika sehemu ya mteremko; *pana bande kubwa* na jito kubwa linalopita karibu na kitovu cha mtaa wenyewe. Jito hili linapitisha *maji machafu kila wakati (uk. 85)* Msisitizo wetu.

Mwaandishi ametumia taashira ya bonde na jito lenye maji machafu kuonyesha vile maisha ya wenyeji wa Kibera yanavyochukiza. Kama anavyosema Mbatiah (1997:8)

> Dhana ya bonde inazua picha ya mahali. Panapotawaliwa na giza, ukungu, ukiwa na mauti. Bonde ni taashira ya ulimwengu ambayo inasisitiza kwamba ni mahali pasipofaa pa kuishi.

Ama kwa kweli, mandhari ya Kibera yanabainisha kuwa hapo si mahali mwafaka pa kuishi. Ni mazingira ambayo yamekiuka ustaarabu unaokusudiwa binadamu. Wanaudhanaishi vilevile wameusawiri ulimwengu kama mahali pasipofaa pa mwanadamu kuishi. Bali na kuwa na msongamano wa mabanda, wanapaswa kustahimili harufu ya kisonzo inayotokana na lile jito la maji machafu. Mara nyingi binadamu hujikuta katika hali fulani isiyotamanika. Ingawa hakuchagua hali hiyo, analazimika kushikamana nayo, kwa vile hana uwezo wa kutengana nayo. Hii ndiyo hali ambayo inampata Richard anapokaa Kibera. Harufu ya kisonzo inamsumbua na kumkirihi moyo hasa wakati wa chakula, lakini inambidi azoee. Wenyenji wa Kibera hawana kazi maalum. Wanategemea vibarua ambavyo havipatikani kwa urahisi (uk 86). Kwa sababu hiyo, inawabidi wachochole wa Kibera kukaa njaa wakati mwingine. Aidha, kuna ukosefu wa huduma za kimsingi kama vile umeme na vyoo. Hata mavazi ya kujisetiri ni haba. Richard anapotembea, anawaona watoto wawili ambao wamevalia visharti tu bila suruali. Vishati vyenyewe ni mararu. Vimeraruka na kuviacha vitumbo vyao wazi. Wadhanaishi hutilia mkazo mateso ya wanadamu sawa na anavyofanya Wamitila kwa kutuchorea picha hii ya Kibera.

Kwa ujumla, picha ipatikanayo katika mtaa wa Kibera Laini Saba ni ya kutamausha. Shida na dhiki za mtaa huu hazielekei kuisha. Richard anaeleza kuwa picha aliyokuwa nayo kuhusu jiji la Nairobi (baada ya kukaa katika mtaa wa Kibera) ilikuwa tofauti na aliyoiona. Anasema:

> Hili lilikuwa jiji la dhiki… jiji la karaha…
> Jiji la uvundo. Labda ndio sababu Kenyatta alikazania watu warudi mashambani (uk 86)

Mwandishi ametumia tabaini kuweka wazi uduni wa maisha katika Kibera. Mtaa huu umezungukwa na majumba ya kifahari ambamo wanakaa watu wenye uwezo. Tunafahamishwa kuwa 'Mtaa wa Kibera Laini Saba umebaidika kama ardhi na mbingu na mitaa inayouzunguka (uk 85). Bali na kusisitiza uchochole wa wakaazi wa Kibera, majumba hayo yanatufanya

tufahamu kuwa jamii inayozungumziwa ina matabaka. Kuna wachache wenye uwezo wa kiuchumi na kuna maskini walio wengi. Mfumo wa uchumi unaohimiza kuwepo kwa matabaka ni ule wa ubepari ambapo nyenzo za kuzalisha mali huwa zimemilikiwa na wachache. Wale wengi wasiomiliki nyenzo za kuzalisha mali hubakia maskini na maisha yao huwa ya kusumbuka. Usumbufu wa binadamu hutiliwa mkazo na wadhanaishi.

Mwandishi ameonyesha kuwa maisha ni mapambano. Katika maisha mwanadamu hana budi kupambana na mambo mengi. Katika mapambano hayo, mtu huwa peke yake. Richard anapomsubiri mwenzake katika uwanja wa magari ya abiria huko Machakos, anashuhudia wasukuma rukwama ambao wanazozania mteja. Mwishowe wanapigana. Ingawa kuna watu wengi ambao walikuwa hapo wakati wa vita hivyo, hakuna aliyeelekea kujali. Jambo hili linamshangaza Richard na anafikia uamuzi kuwa huo ulikuwa mfano bora wa maisha ya viumbe duniani. Tunaelezwa:

> Kila mtu anapigana na mtesi wake kila wakati ilhali kuna nguvu ambayo ilimzunguka, nguvu yenye uwezo wa kuingilia kati na kuamua utesi huo. Lakini ilipenda kubaki au kujiweka kando; nguvu iliyokuwa wasta katika matatizo ya binadamu. Imemwacha huria apambane na mtesi wake (uk 84).

Kulingana na dondoo hili, tunafahamu kuwa ni lazima mwanadamu akutane na matatizo ya aina fulani maishani. Katika kutafuta suluhisho, binadamu huwa hana wa kumsaidia. Lazima apambane peke yake. Mawazo haya yanaafikiana na ya wadhanaishi ambao wanasisitiza kuwa binadamu yuko ulimwenguni kupambana nao pasipo kutegemea usaidizi kutoka mahali popote. Kila kiumbe hakina budi kujipigania ili kiweze kuendelea na maisha. Huu ndio ujumbe anaopata Richard anapopitia mahali panapouziwa manasi. Tunaelezwa:

> Nzi. Nyuki. Binadamu. Wote walikuwa katika kinyang'anyiro cha kujitafutia. Ole wake yule angemuudhi mwenzake (uk. 100)

Viumbe hao wamesawiriwa wakiwa katika harakati za kupambana na maisha. Maisha kama hayo ambapo viumbe kadhaa wanang'ang'ania kitu kimoja bila shaka ni maisha magumu na yasiyotamanika. Hakuna kiumbe ambaye anamsaidia mwingine. Ili kusisitiza hoja kuwa binadamu yu pweke bila msaada wowote uilimwenguni, Wamitila anaonyesha kuwa madhila ya mwanadamu hayatatuliwi hata na Mungu. Shida za Richard zinapomlemea, anamkimbilia Mungu. Mary vilevile anaokoka ili ajiepushe na aibu ya mimba. Hata hivyo, shida zao hazikupata suluhu kwani ukweli wa mimba ya Mary ulijulikana. Nazo juhudi za Richard za kuwa na familia kielelezo kwa kuilea kwa njia ya Kikiristo zikaambulia patupu baada ya bintiye kupata mimba.

Mwandishi huyu anaelekea kusema kuwa ni lazima mwanadamu ayashughulikie maisha yake pasipo kutegemea msaada kutoka mahala popote au nguvu zozote zile.

Wamitila anadhihirisha kuwa maisha hayana maana kwani yametawaliwa na ukatili na vurugu. Mjini Machakos, kwenye uwanja wa magari tunaona kuwa hakuna utaratibu wowote. Uwanja huo umejaa zogo. Kuna wasukuma rukwama ambao wanapita huku wakiwagonga watu bila kujali. Hawa, wanakorofishana kwa sababu ya mteja na wanaishia kupigana. Waliokuwa karibu wanashangilia sokomoko hilo badala ya kuwaamua. Vile vile, huu ni uwanja ambao una hamkani nyingi. Kuna makelele ya vijana wanaopiga mabati ya magari, kelele za magari yanayonguruma kuwahadaa wasafiri, na vijana wanaochuuza. Kila mtu anashughulika kivyake katika harakati za kujitafutia riziki. Huu ni ukosefu wa mpango na ubinafsi pia. Sifa mojawapo ya udhanaishi ni kuvurugika kwa mambo au kukosekana kwa mpango. Haya ndiyo tunayaona katika uwanja wa magari wa Machakos na ni athari ya udhanaishi.

Aidha hakuna mpango katika nyumba ya mwalimu Birundu. Ndani, vitu havijapangwa. Tunaambiwa kuwa vitabu na karatasi mezani havikupangwa kwa utaratibu wowote. Vingine vilikuwa sakafuni. Mapazia ya dirisha ni madogo. Nje, nyumba yenyewe inakaa kama mahame na ilikuwa vigumu kuamini kuwa kuna yeyote aliyeishi pale. Tunaambiwa:

> Labda aliyeishi humo alielewa fika kuwa maisha ya binadamu yamo katika mpito tu ... (uk 69)

Kutokana na dondoo hili tunapata ujumbe wa mwandishi kuwa maisha ya binadamu humu duniani ni ya muda tu. Binadamu anapitia duniani akielekea kaburini. Haya ni mawazo sawa na ya wadhainishi wanaoamini kuwa kifo ni sehemu ya maisha ya binadamu. Hivyo maisha duniani ni ya muda tu.

Kupitia kwa maisha ya Richard, riwaya hii inayasawiri maisha kama adhabu. Maisha yanawaadhibu wanaoyaishi kwa njia mbalimbali. Akiwa shuleni, Richard anapata ugonjwa unaomsumbua sana. Kana kwamba hiyo si adhabu tosha, babake anafariki anapofanya mtihani wa kidato cha nne. Tukio hilo linaathiri matokeo yake. Baadaye anaamua kutafuta kazi huko Nairobi. Anaishi mtaa wa Kibera ambapo anagundua kuwa maisha hayakuwa vile alivyotarajia. Kwa wenyeji wa Kibera, maisha yamewaadhibu kweli kwani wanaishi kinyama. Wanaishi kwenye vibanda, wanasongwa na njaa, hawana kazi, wamezingirwa na uchafu wa kila aina na hata vyoo hamna. Ni maisha yanayokirihi na kutamausha. Richard anapoendelea na kutafuta kazi anapata vibarua tu ambavyo havidumu. Baada ya kupoteza kibarua katika kampuni ya Yakuza Tourists' Firm, alihisi kuwa maisha ni adhabu. Tunaelezwa:

> Alikuwa taabani; sasa alishajiunga na wenzake ambao wameshaongezeka mjini. Wote wana tamaa na kiu ya aina moja – kupata kazi. Hakuwa na matumaini. Alishangaa ni kwa sababu gani mambo yake yakaenda mvange yalivyokwenda. Labda maisha ni adhabu. (uk 151)

Hoja hii ya kuona maisha kama adhabu ni athari ya wadhanaishi ambao hutilia mkazo mateso ya binadamu ulimwenguni. Ameoyesha kuwa maisha ya binadamu yamesongwa na matatizo yaaliokithiri. Wakati Richard na Mary walipokutana na wakasalimiana huko Machakos, waliokuwa kando hawakushughulika, iliwapasa washughulikie shida zao kwanza. Tunaambiwa:

> ... ya ulimwengu wa kesho yangesubiri kwa sababu dharura yake haikuwepo kwa sasa; *iweje sasa wakati wana lukuki ya matatizo ya kuweza kuwatia kichaa?* (uk 164)

Mwandishi ametumia swali la balagha kutufanya tutafakari juu ya matatizo mengi yanayoandama maisha ya mwanadamu. Waaidha, anaona kuwa maisha ya mwanadamu yamekosa furaha. Shida chungu mbovu zinazoandamana na maisha huyafanya yakose furaha.

Shida hizo zinadhihirika katika nyanja mbali mbali za maisha ; asasi ya ndoa ikiwemo. Ndoa nyingi ambazo mwandishi amezungumzia ni za kutatisha tamaa.

Bethsheba, rafikiye Susan, anakiri kwamba ndoa ni mateso tupu (uk. 137). Anajuta kuolewa mapema kwani bwanake hakuzijali hisia zake. Anamwambia Susan kuwa 'Laiti ningejua nisingekimbilia maisha ya ndoa' (uk 138).

Ndoa kama hii iliyojaa majuto inavunja moyo. Vilevile, ndoa ya Deogratias si ya kutamanika. Ingawa wanaohusika wana mali, kuna tatizo kwa kuwa bwana Deogratias ana jicho la nje. Kuna vurugu katika ndoa. Wanafunzi walieneza uvumi kuwa mwalimu Boniface Ngewa alipigana na mkewe kila jioni. Ndoa nyingine ambayo imekumbwa na matatizo ni ile ya Richard na Mary. Harusi yao inakuwa ya kuwakatisha watu tamaa. Walihudhuria wakiwa na matarajio kadhaa: kwamba ingekuwa sherehe yenye raha na tafrija na kwamba wangekula washibe na wakinai. Hata hivyo waiporudi makwao waliibeza harusi hiyo kwa kuwa matarajio yao hayakutimia. Isitoshe, ndoa hii ilijengeka katika msingi dhaifu wa ubinafsi. Mary alitamani sana kuolewa ili ajiepushe na aibu ya kupata mtoto nje ya ndoa. Ingawa alijua kuwa alikuwa na mimba ya Deogratias, hakumwambia Richard.

Baada ya Mary kujifungua, Richard anagundua kuwa bibiye 'mcha Mungu' kamdanganya. Richard anakasirika na kuonyesha hali ya kutamauka kwa sababu mbili. Kwanza, mtoto

aliyezaliwa hakuchukua sura ya wazazi wake. Kinyume na matarajio ya Richard. Pili matamanio yake ya kupata mtoto wa kiume hayakutimia. Haya yalimsononesha na akashindwa kumsamehe bibi yake. Licha ya kuwa ndoa ya Kikiristo, inaonyesha kutofaulu kwa asasi ya ndoa. Mary anapigwa na bwanake kiasi cha kuwa na kovu. Vilevile hana uhuru wowote. Hawezi hata kuwatetea watoto wake. Haya ni mambo yanayosikitisha. Kwa ujumla mwandishi anaonyesha kuwa maisha ya ndoa yametawaliwa na matatizo, hayana furaha na yanakatisha tamaa.

### 3.1.4 Dini

Kulingana na Njogu na Chimerah (1999:14) wadhanaishi hujihusisha na uchunguzi unaohusu uhusiano wa binadamu na Mungu. Dini ni imani katika nguvu zilizo juu ya uwezo wa binadamu. Dini inayozungumziwa katika riwaya hii ni ile ya Kikristo ambapo watu wanaoamini au kutoamini Mungu. Dini hii imesawiriwa kwa njia inayokatisha tamaa. Ni baada ya kusongwa na kulemewa na madhila ambapo mwanadamu anamkimbilia Mungu. Hii ni athari ya udhanaishi. Kiudhanaishi, dini ni chombo cha kumtuliza binadamu anayeteswa na ulimwengu. Inampa matumaini ya siku zijazo katika ufalme wa Mungu (Magare 2002:28)

Akiwa mwanafunzi, Richard hakuona maana yoyote ya dini. Alichukia sana mahubiri. Kilichompeleka kanisani ni kupata fursa ya kukutana na wenzake kwa mazungumzo ".... alielewa kanisa kama mahali pa makutano" (uk 57)

Baada ya kusumbuka sana akitafuta kazi bila mafanikio na kuachwa na mchumba wake, Richard anagundua kuwa hawezi kujitoa katika tope hilo la usumbufu. Anaamua kumhusisha Mungu katika maisha yake ili waweze kumwondolea dhiki maishani. Hii ni baada ya kumsikiliza mhubiri mmoja huko Uhuru Park. Kutokana na mahubiri hayo, tunapata taaswira ya ulimwengu kama mahali pasipofaa kwa sababu ya taabu ainati. Ulimwengu umesawiriwa kama ambao umejaa ukatilii, uzinzi, uhuni na ukahaba, ukosefu wa kazi, vita, mimba zisizotakikana na kadhalika. Haya yanafanya waja wakose matumaini. Huu ni udhanaishi. Ni wengi ambao wamekumbwa na matatizo. Mhubiri anapotoa wito kwa waliosumbuka na kulemewa na matatizo

kuyatua kwa bwana, wote waliokuwamo wanaitikia wito huo. Richard hakuachwa nyuma. Alimwasilishia Mungu shida zake. Ingawa mwanzoni alichelea, Mary Kasiva naye anamua kuyatoa maisha yake ambayo yalikuwa yashavurugika kwa Bwana. Mary alishindwa kuendelea na masomo yake kwa kukosa karo. Aliaajiriwa nyumbani kwa Deogratias. Baada ya muda, anaanza uhusiano wa kimapenzi na mwajiri wake. Anapata mimba, kisha anaiavya. Hata hivyo, wanafumaniwa na bibi yake Deogratias na Mary anafukuzwa huku akiwa na mimba nyingine. Anahangaika sana (uk 167).

Anatafuta faraja katika dini. Alimwomba Mungu ampe bwana ili asipate mtoto nje ya ndoa, jambo ambalo ni aibu kwa Mkristo. Tunaelezwa kuwa tangu aokoke, ombi lake lilikuwa moja tu:

> ...alimwomba Mungu wake amsaidie kumpata mwanaume wa kumwoa na kumkwepesha na kumweposha na fedheha iliyoelekea kumgubika (uk 168).

Lengo lake hasa la kuokoka lilikuwa kujieupusha na aibu. Ndiposa anamshukuru Mungu kwa "kumwonyesha kimbilio, mahali pazuri pa kustakimu na kujikwepesha na fedheha kubwa (uk. 177)". Baada ya kuokoka, maisha ya Richard yanachukua mwelekeo mpya. Nia yake inakuwa kumtumikia Bwana. Kwake mambo yote yalimtegemea Mungu na ndiposa anamwomba ampe mwanamke mzuri wa kuoa.

Mwandishi anaibeza dini na kuonyesha kuwa hata huyo Mungu anayeaminiwa si wa kutegemewa. Richard aliamini kuwa maombi yake ya kutunukiwa bibi mzuri yangejibiwa na Mungu. Kinyume na matarajio yake, anamwoa bibi ambaye ana mimba ya mtu mwingine. Isitoshe, Mary alikuwa mshirikina. Tunamwona akimfukuza bundi kwa kigae na kijinga cha moto. Hii ni ishara kuwa Mary hana imani na dini. Kwake, dini ni ya kumhifadhi tu kutokana na aibu. Mwandishi anaonyesha kwamba licha ya wahusika kuikimbilia dini ili shida zao zitatuliwe dini imeshindwa, hivyo inakatisha tamaa.

Richard anajizatiti kuilea familia yake katika misingi ya Kikristo, ili iwe mfano wa kuigwa. Matokeo ya juhudi za Richard ni mimba ya binti yake Rosylne akiwa katika kidato cha pili. Hili ni jambo la kuvunja moyo hakika. Richard anafikiria kuwa mafundisho ya dini pekee yalitosha kuwa msingi wa malezi mema, Lakini tunaona kuwa dini imeshindwa. Susan anawalaumu wazazi wake kwa malezi mabaya. Anasema:

> Kama kuna makosa yoyote yamo katika malezi mliyotupa. Mmekazania tuyafuate mafundisho ya Biblia bila ya kutuelekeza katika maisha halisi ya ulimwengu huu (uk 196)

Vilevile, Mary Kasiva aliikimbilia dini ili ajiepushe na fedheha ya mimba nje ya ndoa. Siri yake haikudumu kwa kuwa mtoto alipozaliwa, ilijulikana mara moja kuwa hakuwa wa Richard. Kwa mara nyingine dini ikashindwa. Isitoshe mwandishi anaonyesha kuwa dini imeshindwa kuwafanya watu wawe waadilifu. Hata wanaoifuata si waadilifu. Richard ambaye ni Pasta ana hasira za mkizi. Bintiye anapofukuzwa shule, Richard anaghadhabika. Anampiga kinyama huku akimtusi (uk 193). Pasta huyu amejawa na ubinafsi. Aliwashurutisha binti zake kufanya mambo fulani ili apate sifa au asiaibike. Aidha huyu Pasta si msamehevu. Anapogundua kuwa mke wake kamdanganya, anashidwa kumsamehe. Kwa kejeli, tunasimuliwa:

> Alishidwa kumsamehe mke wake. *Mtumishi wa Mungu aliyesisitiza faida na thamani za huruma katika maisha na aushi za binadamu aliwiwa vigumu* (uk 83)

Inakatisha tamaa kuona kuwa hata viongozi wa dini wameshindwa kutekeleza mahubiri yao. Richard ana taasubi ya kiume. Anawadharau na kuwachukia wanawake. Susan anapoamua kumtetea mnuna wake, babake anakasirika sana na anamwambia kuwa hajawahi kutolewa maneno na mwanamke (uk 197). Anawaona kama vishawishi vya uovu (uk 7).

Kule hospitali, Richard alipokuta kuwa amezingirwa na wanawake, anahisi chuki nyingi. Tunaelezwa:

> Aliwatupia macho watu wote waliokuwa pale chumbani. Manesi watatu, mkewe Mary na kitoto chao. Wote wanawake. *Chuki iliyokuwa imefichama kwenye akili yake ilivundumka kama zaha za volkeno* (uk 183)

Tunatamauka kuona kuwa dini ambayo inapaswa kudumisha maadili katika jamii imeshindwa. Kama viongozi wa dini wameshindwa, sembuse "kondoo"?

Huenda ni kwa sababu ya kushindwa huku ambapo dini hii inapigiwa maswali. Wahusika wengi wana tashwishi kuhusiana na dini. Ni kana kwamba wanasaili kuwepo kwa Mungu. Hii ni athari ya udhanaishi. Kabla Richard aokoke anashuhudia kisa ambacho kinamfanya adadisi kuwepo kwa Mungu. Kijana aliyeiba kibogosho anauawa. Richard anajiuliza iwapo Mungu alikuwa anaona ukatili ulioendelezwa na waja. Anapoinua macho yake juu, yanapofushwa na jua, hivyo asione chochote. Hii ni ishara kwamba hasadiki katika Mungu. Bosire naye, mwanafunzi wa chuo kikuu hana imani dhati na dini. Ana maswali mengi kuihusu, sawa na wanafunzi wengi wa chuo kikuu, kwake dini ya Kikristo ni "sehemu ya fasihi ya kimapokezi ya mataifa ya mashariki ya mbali" (uk 145).

Ingawa Susan hakubaliani na maoni ya Bosire, anakiri kuwa misingi ya imani yake ilikuwa ishaanza kutikisika, na akauona upungufu uliokuwapo katika mwito wa baba wa nguvu ya sala. Susan anamdhihaki 'Mungu wa siku hizi' ambaye alionekana kupenda pesa badala ya kafara za hapo awali. Kwa dharau Susan anawaza kuhusu dini:

> Hivi leo mambo yalishabadilika kabisa. Watu hawakuwa wakichinja wanyama ila walitoa sadaka za pesa. *Yaelekea aliyekusudiwa hakuwa na haja ya nyama tena; keshazikinai sasa alitaka sadaka tofauti (*uk 112)

Nukuu hii inatufanya tujiulize ni Mungu gani huyu ambaye anabadilika badilika?

Wamitila ameisawiri dini kama chombo cha kudhulumu na hivyo kuongeza mateso katika maisha. Kwa kusingizia dini, watoto wa Richard wanapigwa, wananyimwa uhuru wa kucheza na wenzao, kucheka na hata kujichagulia. Kila mara wanakumbushwa kuwa ni watoto wa nyumba ya Kikristo (uk 61) Jambo hili linawafanya waishi katika woga. Hizi ni adhari za udhanaishi Isitoshe dini imesawiriwa kama chombo kinachotawanya jamii.

Baada ya Roselyn kutunga mimba, anafukuzwa na babake kwa sababu alikuwa amemwaibisha mtumishi wa Mungu. Susan anamwambia babake kuwa "imani inayovunja mji haitufai" (uk 198). Inaonekana kuwa dini imekosa maana katika jamii iwapo itaongezea jamii shida badala ya kuwa suluhisho.

Mwandishi, kupitia kwa Susan, anashauri kuwa ni lazima mahuluku akabiliane na shida zake vilivyo pasipo kutegemea nguvu zozote zile. Susan anawaza na kujiuliza iwapo nguvu ya sala tu ingetosha kusuluhisha masaibu katika jamii. Anajisaili kuhusu mwito wa nguvu ya sala uliokazaniwa na babake:

> Je, ulikuwa wa kufaaa au ulikuwa tasa? Je, matatizo mangapi ambayo yangesuluhishwa kwa mwito huo? Umaskini uliowavaa watu nchini kama kubega, tofauti zilizokuwapo kati ya matajiri na maskini, udhalilishwaji wa wanawake katika jamii yetu. *Nguvu ya Sala?* (uk 199).

Maswali ya balagha yametumika kumfikirisha msomaji juu ya dhiki za mwanadamu na kushindwa kwa dini katika kukabiliana na dhiki hizo. Mwandishi huyu anatoa rai kuwa shida hizi za kijamii zitatuliwe na mwanadamu mwenyewe wala asikubali kupofushwa na dini. Susan anahisi kuwa babake amefeli katika malezi kwa sababu ya imani katika dini. Mwandishi anatoa hoja hii kupitia kwa Susan. Susan anasimulia kuwa "kwa kiasi kikubwa imani hiyo ilishampofua na kumfanya ashindwe kuuangalia uhalisi" (uk. 188).

Hoja inayojitokeza katika dondoo hili ni kwamba dini haifai kuwa kisingizio cha mja kutokabiliana na uhalisia wa maisha yake. Ni hoja inayooana na ya mdhanaishi Camus, aliyetoa rai kuwa dini ni kama kasumba ambayo imempofusha binadamu asione ukweli. Hivyo basi yeyote anayetaka kujua ukweli wa maisha hana budi kujitenga na imani na falsafa za kidini, akabiliane na hali yake iliyo. Huu ni udhanaishi.

Dini imefaulu katika kuwakengeusha wafuasi wake. Richard amejitenga na wazee wengine wa kijiji. Anawaona kama ambao watu wanaoishi gizani, ilhali yeye ameona nuru ya wokovu. Tunasimuliwa:

> Alielewa jinsi maisha yake yalivyokuwa tofauti na ya wazee hawa. Wazee waliovuta ugoro. Wazee waliovalia magwanda uchwara na waliodidimia katika giza nene (uk. 5)

Kwa sababu ya kujitenga huku, alichukiwa na baadhi ya wanakijiji. Kwa vile amekengeushwa na dini, anadharau mila na tamaduni za jamii yake. Anajaribu kuukata mkuyu ambao kulingana na utamaduni ulikuwa madhabihu. Mwandishi anaonekana kuidhihaki dini. Juhudi za Richard za kuukata mkuyu ziliambulia patupu. Nyoka mkubwa anajitokeza wakati Richard anapojaribu kuukata ule mti.

Bali na kujitenga na jamii, Richard ameitenganisha familia yake na jamii. Watoto wake hawaruhusiwi kutangamana na watoto wengine, hasa wale ambao familia zao si za Kikristo. Richard amekengeushwa na dini, naye akaikengeusha familia yake. Ukengeushi ni sifa mojawapo ya udhanaishi.

Kwa ujumla, tunaona kuwa dini inakatisha tamaa kabisa. Imeshidwa kuleta nafuu yoyote kwa maisha ya waja yaliyojaa dhiki. Wanaoikimbilia wakiwa na matumaini wanavunjikiwa.

Matarajio yao hayatimii. Inaelekea mwandishi anawakashifu wanaojificha katika dini wakati wa shida badala ya kutafuta suluhisho halisi. Ni jambo la kusikitisha sana kuona kuwa dini inahusishwa na sifa mbaya kama vile ukali, hasira ubaguzi, ukandamizaji na kadhalika. Hakika dini inatamausha.

### 3.1.5 Kifo

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999: 15), kifo ni mojawapo ya maudhui yanayoshughulikiwa na waandishi wa kidhanaishi. Kwao, kifo ni sehemu ya maisha ya binadamu.

Japo kwa ufupi, Mwandishi ameangalia suala la kifo. Ameonyesha kuwa maisha ya mwanadamu hutawaliwa na hofu ya kifo. Mawazo ya binadamu kuhusu kifo daima huandamana na woga. Katika jamii ya Richard, mlio wa bundi ulihusishwa na kifo. Mlio huo uliwatia hofu wanajamii. Nzisa (mamake Richard) anapousikia mlio huu, anapatwa na hofu kubwa, hasa huu ukiwa ni wakati ambapo bwanake ni mgonjwa sana. Ni kana kwamba bundi aliaminika kuwa mjumbe wa kifo. Tunaelezwa:

> Watu walimwogopa bundi *labda walichokiogopa ni kile alichohusishwa nacho: kifo.* Nyumba nyingi zilizovimbwa na nyasi zilikuwa na vigae vya vyungu kwenye vilele vya mapaa yake. Waliamini kuwa yule ndege asingeweza kutua juu ya nyumba iliyokuwa na paa lenye gae la chungu (uk.51).

Ni wazi kuwa watu wanakiogopa kifo na wanafanya juhudi sana kukiepuka. Mzee Nzimba anapokuwa mgonjwa, mengi yanafanywa ili asife. Anapelekwa kwa Daktari pamoja na waganga. Hata hivyo, kifo kinadhihaki juhudi hizo zote na kinapata ushindi. Nzimba anafariki. Udhaifu wa mwanadamu pamoja na hali ya kukata tamaa inajitokeza. Mja ametamauka kwa kuwa hana uwezo juu ya kifo. Baada ya kifo cha Nzimba, hali ya kukata tamaa inatawala. Tunaelezwa:

> Mwanzo, ukimya wa kutisha ulitawala kile chumba. Kifo kilitembea mle kikinesa na kudesa kwa shauo la ushindi. Kiliporidhika na kazi yake, kilitoweka kuelekea kwingineko kulikohitajika huduma zake (uk. 53).

Mwandishi ametumia tashhisi akakihuhisha kifo. Anakipa uwezo wa kutembea na kuringa kwa sababu kina uwezo juu ya binadamu. Kwa kuzungumzia kifo kama kitu kilicho na uhai, mwandishi anakipa ile sifa ya kuwa sehemu ya maisha ya binadamu. Huu ni udhanaishi. Wadhanaishi hushikilia kuwa kifo ni sehemu ya maisha au daraja nyingine ya maisha.

Aidha, kupitia kwa ndoto ya Richard iliyotangulia tanzia ya kifo cha babake, mwandishi anaonyesha kuwa kifo ni fumbo, kifo kinamtisha na kumtawala mja. Katika ndoto hiyo, Richard anaona nyama la kutisha lenye ulimi ulioadikwa maneno yasioyoeleweka. Upande wa kushoto wa ulimi huo ulikuwa na neno MORTIS. Hili ni neno la kilatini lenye maana ya kifo. Kwenye upande wa kulia, neno ANGST lilionekana. Maana yake ni kihoro. Hata Richard anapojaribu kujisalimisha kutoka kwa nyama hili, anashindwa kwa mara nyingine, maisha yanaonekana kutawaliwa na fadhaa ya kifo. Binadamu anavunjika moyo anapofahamu kuwa hatima yake ni kifo na hana njia ya kukikwepa.

## 3.2 ATHARI YA MAZINGIRA KWA MWANDISHI

Kama tulivyosema hapo awali katika sura ya pili, nadharia ya kisosholojia husisitiza kuwa ni muhali kuihakiki kazi ya msanii nje ya muktadha wa mazingira yaliyoizaa kazi hiyo. Mazingira yaliyomzunguka mtunzi hadi wakati wa kuitunga kazi yake huwa na athari ambazo hujitokeza katika kazi aliyoitunga. Ni katika muktadha huu ambapo tutaangazia baadhi ya mazingira ambayo Wamitila alikumbana nayo, yakamfanya aiandike riwaya hii ya *Nguvu ya Sala.*

Mwandishi huyu alizaliwa nchini Kenya. Nchi hii kama nchi nyingi za Kiafrika ilikumbwa na matatizo tangu enzi za wakoloni. Wananchi walikandamizwa kwa muda mrefu kabla ya

kuzinduka na kupigania uhuru wao. Walifanikiwa kuivunja minyororo ya Wakoloni mnamo mwaka wa 1963, kufuatia vita vikali. Baada ya uhuru ilitarajiwa kuwa maisha yangechukua mkondo mpya ambapo unyanyasaji, ubaguzi na maovu mengine yangekuwa mambo ambayo yamepitwa na wakati.

Hata hivyo, mambo haya yaliendelea. Baada ya miaka mingi ya utawala usioridhisha, baadhi ya viongozi waliwaongoza wananchi kudai haki zao. Walitaka kuanzishwa kwa siasa za vyama vingi badala ya chama kimoja ambacho kilitumiwa kuwanyima wananchi haki zao. Hili halikukubaliwa kwa urahisi na wale viongozi ambao walijitakia makuu. Msururo wa maandamano ambayo yalisababisha vifo vya watu kadhaa ulifuatia. Mwishowe, siasa ya vyama vingi ilikubaliwa. Kwa mara ya kwanza, serikali ya Kenya ikawa yenye vyama vingi baada ya uchaguzi uliofanyika mnamo mwaka wa 1992.

Matarajio ya watu yalikuwa kwamba demokrasia ya vyama vingi ingeleta haki na usawa. Mwandishi Wamitila aliiandika kazi yake baada ya kuanzishwa kwa siasa za vyama vingi nchini. Yumkini mambo aliyoyashuhudia ndio yaliomfanya aandike riwaya inayoegemea mtazamo wa kidhanaishi. Shida ziliwakumba wananchi katika nyanja mbalimbali za maisha. Huduma za kimsingi ziliendelea kuwa adimu kwa mwananchi wa kawaida. Umaskini, hasa sehemu za mashambani uliwafanya wananchi wengi kuhamia mijini kutafuta ajira. Hata huko haikuwa rahisi kupata kazi. Hii iliwapelekea wengi kuishi katika mabanda huku wakitafuta kazi. Miji ikawa na mitaa ya madongoporomoka. Maisha kwa walioishi huku yalikuwa ya kukatisha tamaa. Mara nyingi watu walikosa chakula. Kupata mavazi ikawa shida. Maji safi pamoja na vyoo vilikosekana. Matatizo kama haya yaliwapelekea watu kuishi maisha ya ufasiki. Haya ndiyo maisha ambayo Wamitila anatusawiria katika mtaa wa Swahili na ule wa Kibera Laini Saba.

Maisha kama hayo hayakufaa kwa wananchi ambao walikuwa katika nchi yao chini ya utawala wa viongozi wao. Mwandishi analaumu mfumo wa kijamii na kiuchumi kwa maisha duni ya watu. Kupitia kwa Susan, mwandishi anasema:

> Watu hawakuyatenda waliyoyatenda kwa mapenzi
> yao bali yalikuwa matokeo ya wakati na mfumo wa kijamii na kiuchumi uliokuwapo (uk. 184).

Haki na usawa uliotarajiwa baada ya demokrasia ya vyama vingi haukufikiwa. Jamii ya mwandishi ina matabaka. Kuna matajiri wachache wanoishi kwenye majumba ya kifahari na wachochole wengi wanaishi kwenye madangoporomoka. Picha ya Kibera Laini Saba na mtaa iliyouzunguka kama vile Otiendo, Ngumo na Onyoka ni ithibati.

Aidha, unyanyasaji uliendelezwa na serikali na wenye nguvu kiuchumi. Tunaona kuwa serikali inatumia vyombo vya dola kuikandamiza kampuni ya yakuza Tourists' Firm baada ya kampuni hii kushindwa kuonyesha kuwa serikali haikuhusika na mauaji ya Watalii. Nao wenye nguvu kiuchumi kama vile mfanyi biashara Naipul wanawadhulumu wafanyikazi wao. Richard anafutwa kazi bila sababu maalum. Tunavunjika moyo kuona kuwa miaka mingi baada ya uhuru, wananchi wa Kenya walidhulumiwa na Wahindi waliokuwa na uwezo wa kiuchumi.

Matatizo mengi ya kiuchumi na kijamii yaliwasukuma wengi kutafuta faraja katika dini. Madhehebu mengi yalianzishwa na mikutano ya mahubiri huko uhuru park ya mara kwa mara ilihudhuriwa na watu wengi. Wahubiri wengine walichukulia dini kama njia ya kujipatia riziki. Walianzisha mahubiri ya alasiri. Baada ya mahubiri waliwashauri waliosikiliza kumtolea Mungu sadaka. Wamitila alishuhudia mambo kama haya na yalimwathiri. Hii ndiyo sababu anaibeza dini na kuisawiri kwa njia isiyotamanika. Wahusika wengi kama vile Richard na Mary wanakimbilia dini ili wapate kuepuka shida zinazowakabili maishani, lakini dini inafeli kuwasaidia.

Waaidha, msanii huyu huenda ameathiriwa na kazi za waandishi wa kidhanaishi kama vile Albert Camus na Samuel Beckett ambao waliamini kuwa ulimwengu ni mahali pasipofaa pa mahuluka kutokana na dhiki zinazomkabili. Ni kwa sababu ya athari hizi ambapo Wamitila anamsawiri mhusika mkuu Richard akikumbana na shida ainati maishani mwake.

Mdhanaishi Heidegger vilevile amemwathiri mwandishi huyu. Kwake Heidegger, matukio maishani mwa mtu ni sawa na ajali. Mwanadamu hawezi kubadilisha yale ambayo yanatukia. Maisha ni majaaliwa. Huu ndio ujumbe ambao Wamitila anatupasha kupitia kwa maisha ya Richard. Richard ana mpango wa maisha yake na anajitahidi sana kuufanikisha mpango huu. Hata hivyo mambo yote aliyopanga yalimwendea mvange na kumfanya ahisi kuwa maisha yalikuwa adhabu.

Aidha, Wamitila ameathirika pakubwa na wadhanaishi wa Kilimwengu kama vile Jean Paul Sartre na Samwel Beckett. Kama wadhanaishi hawa, Wamitila anadadisi kuwepo kwa Mungu na nafasi ya dini katika jamii. Anaidhihaki na kuiona kama ambayo haina maana yoyote. Mtazamo wa maisha wa mwandishi huyu umeathiriwa na Kezilahabi. Kama asemavyo Mbatiah ( 2003:17) mwandishi huyu amechukua mtazamo unaofanana na wa Kezilahabi kuhusu swala la maana ya masha – mtazamo wa kidhanaishi.

Ni wazi kuwa mwandishi huyu aliathiriwa na hali mbalimbali alizozishuhudia katika jamii yake. Anazungumzia mandhari halisi na mambo ambayo wanajamii wake wanaweza kujitambulisha nayo. Aidha, katika harakati zake za usomi, alikumbana na kazi za waandishi wa kidhanaishi ambazo zilimchochea. Yumkini alilinganisha hali ya jamii yake na ile iliyozungumziwa na wadhanaishi wengine na akahisi kuwa hakukuwa na tofauti kubwa maishani. Yote yalikuwa maisha yaliyosheheni dhiki. Ni hali na mazingira hayo ya kijamii ambayo yalimpelekea mwandishi kuchukua mtazamo wa kidhanaishi.

## 3.3 HITIMISHO

Katika sura hii tumechunguza athari za udhanaishi katika jamii iliyosawiriwa na mwandishi wa riwaya ya *Nguvu ya Sala*. Tumeona kuwa kuna athari za udhanaishi kwani mwandishi ameonyesha vile maisha ya mja yalivyoandamwa na usumbufu na kutofanikiwa kupitia mhusika Richard. Maisha ya mhusika huyu yamejaa malengo ambayo hayakutimia. Kilele cha kutotimia

kwa malengo yake kinafikia pale anapojaribu kuikuza familia kielelezo cha kuigwa na jamii. Badala yake binti yake anapata mimba na anamfukuza nyumbani. Richard anatamauka.

Inakuwa kana kwamba binadamu ametupwa katika ulimwengu wenye vurugu na usiomjali apambane na madhila pasipo usaidizi wowote. Katika riwaya hii, tunaona kuwa hata Mungu amemwacha binadamu ayatatue matatizo yake kwani wanaomkimbilia wanavunjikiwa na wanaishia kukata tamaa. Kifo nacho kimesawiriwa kama ambacho kimemshinda mwanadamu maarifa na chenye kumjaza hofu maishani. Mja hana hiari juu ya kifo. Inakatisha tamaa kuona kuwa baada ya kusumbuka ulimwenguni, juhudi za binadamu zinaishia kaburini. Kifo kinaathiri hata maisha ya wale wanaishi. Baada ya kifo cha Nzimba, mji wake unasambaratika na mipango ya Richard ya kuendelea na masomo inafikia kikomo. Haya ni mambo ambayo yanavunja moyo.

Ingawa riwaya hii inatufanya tukate tamaa tunapoyafuata maisha ya Richard, tunaona kuwa kuna matumaini kupitia kwa maisha ya Susan. Licha ya vikwazo vingi katika maisha yake, Susan anapata ufanisi maishani. Anafanikiwa kusoma hadi chuo kikuu na hakuangukia katika mitego ya ulimwengu kama dadake Roselyn. Anawekewa mitego na wanaume kama vile Birundu lakini anajinasua.

Kupitia kwa maisha ya Susan, Mwandishi anaelekea kusema kuwa kuna uwezekano wa hali kuwa bora hata katika hali inayotamausha.

# SURA YA NNE

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 4.1 HITIMISHO

Katika utafiti huu, tumeshughulikia riwaya mbili ambazo ni *Kichwamaji* na *Nguvu ya Sala* kwa minajili ya kuchunguza iwapo riwaya hizi zinaweza kuainishwa kama kazi za kidhanaishi. Utafiti wetu umebainisha kuwa riwaya hizi mbili zimeandikwa na wasanii ambao wanaegemea mtazamo wa kidhanaishi. Chembechembe za athari za udhanaishi zimeweza kubainika katika kazi zote mbili. Waandishi wote wawili na hasa Kezilahabi, wanaelekea kuonyesha kuwa maisha ya mwanadamu hapa duniani yamekosa maana, kwa kuwa yametawaliwa na dhiki. Hivyo basi tumeona kuwa riwaya hizi mbili zinaweza kuchukuliwa kama kazi za kidhanaishi.

Hata hivyo, utafiti huu umebaini kuwa viwango vya udhanaishi katika kazi hizi mbili vinatofautiana. Riwaya ya *Kichwamaji* ambayo imeandikwa na Euphrase Kezilahabi, imeonyesha udhanaishi wa hali ya juu. Mhusika Kazimoto amekata tamaa maishani kiasi kuwa haoni haja ya kuishi tena. Anajitia kitanzi. Kezilahabi ameonyesha kuwa hakuna matumaini yoyote ya kuboresha maisha ya binadamu. Mateso, majonzi na kifo ni ukweli ambao mwanadamu anapaswa kuukumbatia maishani mwake. Hii ndiyo sababu mwandishi huyu anatoa rai kuwa kuyatunza maisha yako ndiyo adhabu kali ambayo binadamu amewahi kupatiwa. Kazi hii inavunja moyo kabisa.

Kwa upande mwingine, mwandishi wa *Nguvu ya Sala,* licha ya kuyasawiri maisha yakiwa magumu na yasiyoridhisha kupitia kwa mhusika Richard, ametoa mwanga wa matumaini kupitia kwa mhusika Susan. Hivyo anayeisoma kazi hii havunjiki moyo kabisa, kinyume na ilivyo kwa anayeisoma riwaya ya *Kichwamaji.*

Vilevile, tumejadili jinsi mtazamo wa kidhanaishi wa kila mwandishi ulivyoathiriwa na mazingira mbalimbali. Tumeona kuwa kila mwandishi ameathiriwa na mazingira ya jamii yake, yakiwemo matukio ya kihistoria ya jamii husika. Aidha waandishi mbalimbali walioegemea falsafa ya udhanaishi yamewaadhiri wandishi hawa.

Kezilahabi ameathiriwa na matatizo sugu yaliyoikumba nchi yake ya Tanzania, kabla ya uhuru na miaka saba baada ya Azimio la Arusha. Wakati wa vita vya uhuru, watu walipoteza maisha yao na mali iliharibiwa. Huenda Kezilahabi aliilinganisha hali hii na ile ya Magharibi iliyozua udhanaishi. Katika juhudi za kuleta maendeleo nchini, Azimio la Arusha lilianzishwa mnamo mwaka wa 1967. Miaka Saba baadaye,wakati Kezilahabi aliiandika riwaya yake, matatizo ya Watanzania yalikuwa yanawaandama. Mambo haya yalimwathiri, yakamtamausha na kumfanya auchukue mtazamo wa kidhanaishi. Ameathirika kiasi kuwa haoni matumaini ya kuikomboa nchi yake kutokana na matatizo yanayoikumba.

Wamitila naye, aliona kuwa nchi yake ya Kenya inaendelea kusongwa na dhiki miaka mingi baada ya uhuru. Matatizo sugu kama vile umaskini, matabaka katika jamii, ukabila, wizi na kadhalika yaliendelea miongoni mwa jamii ya Wakenya. Juhudi za kuleta haki na usawa kupitia kwa demokrasia ya vyama vingi zinagonga mwamba. Wamitila aliandika riwaya yake miaka saba baada ya kuanzishwa kwa siasa ya vyama vingi nchini mwake. Hata hivyo, anaonyesha kuwa hali ya maisha ya wananchi wa kawaida iliendelea kudhoofika. Watu wengi wakajiua kifalsafa kwa kukimbilia dini ili wafarijike. Huenda haya ndiyo yaliyomkera msanii na kuyaona maisha kama ambayo hayana maana; mtazamo wa wadhanaishi. Hata hivyo mwandishi huyu ana matumaini kuwa hali nchini Kenya inaweza ikabadilika ikiwa njia mwafaka za kutatua matatizo yaliyoko zitatumiwa.

## 4.2 MAPENDEKEZO

Katika utafiti wetu, tumejibana zaidi katika upande wa maudhui. Tumegusia fani tu pale ambapo ilitusaidia kutilia hoja mkazo. Hata hivyo riwaya hizi zinastahili uhakiki kwa upande wa fani. Riwaya ya *Nguvu ya Sala* hasa imeonyesha ufundi wa hali ya juu katika matumizi ya fani. Hivyo ni mapendekezo yetu kuwa wahakiki wafanye utafiti zaidi unaohusiana na fani katika riwaya

hizi. Aidha, tunatoa rai kwa wahakiki kuzichunguza kazi za waandishi ambao wamekulia katika mazingira sawa ya kijamii ili kubainisha iwapo mitazamo yao ya kidhanaishi itakuwa tofauti au la.

## MAREJELEO


Arege, T.M. (1998) "Ushairi Huru wa Kiswahili: Mchango wa Euphrase Kezilahabi." Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa).

Cruickshank, J. (1958) *Albert Camus: The Literature of the Revolt.* London: O.U.P

Fage, J. na Oliver, R. (1984) *The Cambridge History of Africa.* Australia: C.U.P.

Foulguie, P. (1948) *Existentialism:* London. Dennis Dobson Ltd.

Gachukia E. (1980) "Cultural Conflict in East African Literature". Chuo Kikuu cha Nairobi Tasnifu ya Ph.D, (Haijachapishwa)

Greene, N.N. ( 1960) *Jean-Paul Sartre: The Existentialist Ethic:* USA University of Michigan Press

Heinemann, F.H. (1958) *Existentialism and the Modern Predicament.* New York Harper & Brothers Publishers.

Irungu, C.M (1999) "Dhana ya Maisha katika novela mbili za Euphrase Kezilahabi: *Nagona* na *Mzingile*". Chuo Kikuu cha Nairobi Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa).

Kaufmann, W. ( 1956) *Existentialism From Dostoevsky to Sartre* New York. Meridian Books Inc.

Kenyatta, J. (1978) *Facing Mount Kenya: The tribal Life of the Gikuyu.* Nairobi: Heinemann.

Kezilahabi, E. (1971) *Rosa Mistika.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kezilahabi, E (1974) *Kichwamaji.* Nairobi: East African Publishing House.

Kezilahabi, E (1974) *Kichomi.* Nairobi: East African Publishing House.

Kezilahabi, E (1981) *Dunia Uwanja wa Fujo*: Arusha: E.A. Publications Ltd.

Lepp, 1 (1968) *Death and its Mysteries* London. Burns and Dates.

Lugano, R.S. (1989) Mwanamke katika riwaya za Kezilahabi. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Magare, F ( 2002) "Uhakiki Tamthilia ya *Amezidi* kama Kazi ya Kiubwege". Chuo wa Kikuu cha Nairobi Tasnifu ya M.A (Haijachapishwa).

Mbatiah, M (1998) Mienendo Mipya katika uandishi wa Kezilahabi: *Nagona* na *Mzingile* katika *Mulika* Juzuu Namba 24 *TUKI*

Mbatiah, M (2001) *Kamusi ya Fasihi* Nairobi. Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mbatiah, M (2003) A Critical Aproach to Wamitila's *Nguvu ya Sala* Katika *Hekima* Juzuu 11 No. 1 Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mbiti, J.S. (1990) *African Religions and Philosophy*. Nairobi: Heinemann.

Mulokozi, M. ( 1977) Fasihi na Mapinduzi: Kioo cha Lugha katika *Jarida la Chama cha Kiswahili* Dar – es Salaam

Mungah, C. (1999) "Dhana ya Maisha katika Novela mbili za Euphrase Kezilahabi: *Nagona* na *Mzingile*." Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya M.A (Haijachapishwa).

Musau, P. ( 1985) "Euphrase Kezilahabi: Mwandishi Aliyekata Tamaa". Chuo Kikuu cha Nairobi Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa).

Ngugi wa Thiong'o (1977) *Homecoming:* Nairobi H.E.B. Ltd.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi. Nadharia na Mbinu.* Nairobi: J.K. Foundation.

Nyerere J. K. (1968) *Tanzania Today*. Nairobi: University Press of Africa.

Philips, A. (1953) *Survey of African Marriage and Family Life.* New York: O.U.P

Robert, A (1995) *The Cambridge Dictionary of Philosophy*. U.S.A Cambridge University Press

Senkoro, F. (1982) *Fasihi.* Dar es salam: Publicity Press

Wamitila, K. (1999) *Nguvu ya Sala:* Nairobi Longhorn

Wamitila, K. (2002) *Uhakiki wa Fasihi Misingi na vipengele vyake.* Nairobi. Phoenix Publishers.

Wamitila, K. (2003) *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia.* Nairobi Focus Publications.

Wanjala, C. (1978) "Allienation in Modern East African Literature." Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya M.A (Haijachapishwa).

Warnock, M (1970) *Existentialism.* New York: Oxford Unversity Press.

Wilson, E. na Goldfarb, A. (1991). *Theatre: The Lively Art*. New York: McGraw – Hill.



UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION




JOMO KENYATTA MEMORIAL LIBRARY